SUPA JACKPOT
TZS. 1,093,395,265
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**WAGONJWA** 193 waanza kuchunguzwa virusi Marburg




UKURASA 11

Jumamosi Machi 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581260

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mchakato wa Katiba waiva

UKURASA 2



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro

## Serikali yakazia msimamo kuhusu shule za bweni

UKURASA 2

UKURASA WA 2

### MAZISHI WALIOUNGUA MOTO GESI YAKWAMA

MAZISHI ya watu wawili waliofariki dunia kutokana na ajali ya moto juzi yaligonga mwamba kwa kile kinachodaiwa familia kushindwa kulipa bili inayokadiriwa...

UKURASA WA 3

### WAZIRI AWA MBOGO VIONGOZI MASLAHI

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeagizwa kuwachunguza baadhi ya viongozi wanaojihusisha na vitendo vya mgongano wa maslahi...



Baadhi ya wananchi wakijaribu kumwokoa mwendesha pikipiki aliyezama kwenye mtaro baada ya daraja kufunikwa na maji ya mvua na kusababisha mafuriko katika Kata ya Mkuyuni, Nyamagana mkoani Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa mwalimu wa panya wanaonusa na kubaini mate au makohozi yenye vijidudu vya kifua kikuu, Mariam Chamkwata wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Morogoro katika maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani yaliyofanyika kitaifa jana Bariadi mkoani Simiyu. Wa pili kulia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: OWM**

## Mafuriko yatikisa, barabara zafungwa kwa saa tatu

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA SC, YANGA ZACHANGA KARATA UK. 24

KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk.Hussein Ali Mwinyi akitoa nasaha zake kwa waumini wa dini ya Kiislamu wakati wa hafla ya ufunguzi Masjid Noor (Msikiti Kichaka) kwa Haji Tumbo, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi jana, baada ya kujengwa upya kwa ufadhili wa Shekhe Ali Salim Ali. **PICHA: IKULU**

# Mchakato wa Katiba mpya waiva

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MCHAKATO wa Katiba mpya pamoja na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Uchaguzi unatarajiwa kuanza kufanyiwa kazi baada ya kupitishwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2023/24.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha baraza la wafanyakazi la wizara hiyo kilichofanyika jijini hapa.

Dk. Ndumbaro alisema marekebisho ya katiba yataanza kufanyika baada michakato ya kupitishwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kupitia baraza la wafanyakazi na mwisho kuidhinishwa na Bunge.

"Mchakato wa Katiba mpya ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo ili kufanikiwa unahitaji rasilimali fedha nyingi na wajumbe wa kikao cha baraza la wafanyakazi mtambue mna jukumu hilo la kupitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka huu 2023/24 ili kufanikisha mambo hayo makubwa ya kitaifa," alisema. Kwa mujibu wa Dk. Ndumbaro, hitaji la Katiba mpya ni la Watanzania, hivyo wizara yake inatakiwa kujipanga ili kuhakikisha inakamilisha mchakato huo kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

"Marekebisho ya sheria za uchaguzi hizo yanahitajika pamoja na Sheria ya Tume ya Uchaguzi, hivyo wizara yetu inahitaji rasilimali fedha kupitishwa ili kukamilisha michakato hiyo haraka," alisema.

Alibanisha kuwa mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni Sh. bilioni 36 sawa na ongezeko la Sh. bilioni tisa ya fedha zilizoidhinishwa na bunge kwa mwaka wa fedha unaomalizika.

Pia alisema wajumbe hao wanahaki ya kuongeza au kupunguza mapendekezo hayo ili kukamilisha jukumu walilopewa na Rais kuhusu marekebisho hayo.

Aliyataja majukumu mengine waliyokabidhiwa kuwa ni kutumia majukwaa ya kimataifa kuhusu kuondoa dhana kuwa nchi haiheshimu haki hizo pamoja na kutoa elimu ya sheria kwa wananchi.

Waziri Dk. Ndumbaro alisema kuna mambo mengi yanayoihusu wizara hiyo ambayo yanahitaji fedha ili kukamilisha kwa wakati majukumu hayo makubwa ya kitaifa na kimataifa.

Aidha, aliwataka watumishi kujenga tabia ya kujiwekea akiba kabla ya kustaafu ili kuondoa malalamiko kwa wastaafu.

Dk. Ndumbaro alisema kuna baadhi ya watumishi wamekuwa na tabia ya kuishi maisha ya anasa wakiwa kazini lakini wakistaafu wanakosa akiba ya kuendesha maisha.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo na Katibu Mkuu wa Wizara, Mary Makondo, aliyataja malengo ya baraza hilo kuwa ni kupokea mapitio ya bajeti ya mwaka 2022/23 na mapendekezo ya bajeti ya fedha ya mwaka 2023/24.

Makondo alisema katika kikao hicho pia watajadiliana kwa pamoja masuala ya mafanikio na matatizo katika sehemu ya kazi ili kuondoa malalamiko.

## Mazishi walioungua moto gesi yakwama

**Na Pilly Kigome**

MAZISHI ya watu wawili waliofariki dunia kutokana na ajali ya moto juzi yaligonga mwamba kwa kile kinachodaiwa familia kushindwa kulipa bili inayokadiriwa kufikia Sh. milioni tano katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Juzi na jana ndugu, jamaa na marafiki walikuwa wakijitokeza eneo la msiba, Mabibo, Dar es Salaam kwa ajili ya mazishi lakini baadaye wakiondoka kwa kutolewa kwa matangazo kuwa miili bado haijapatikana.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mabibo Farasi, Andrew Kibuya, aliiambia Nipashe kuwa walishindwa kuzika jana kutokana na familia kushindwa kulipa deni kubwa la matibabu katika hospitali hiyo.

Alisema bili hiyo ilikuwa kubwa kutokana na gharama za matibabu kwa majeruhi, gharama za chumba cha wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU) na sehemu ya kuhifadhia maiti baada ya majeruhi hao kupoteza maisha.

"Bili hiyo ilikua ikikua siku hadi siku kutokana na gharama hizo kwa majeruhi wote wawili mara baada ya kufikishwa hospitalini hapo kwa matibabu," alisema.

Kutokana na hali hiyo, uongozi wa serikali ya mtaa ulichukua uamuzi wa kuandika barua ya kuomba msamaha ili kupata miili hiyo lakini hadi jana mchana walikuwa hawajapata ridhaa.

Hata hivyo, Kibuya aliiambia Nipashe wana imani kubwa hospitali hiyo watawakabidhi miili hiyo kwa kuwa walikuwa wakishughulika na mambo hayo mara kadhaa.

Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi wa MNH, Redemptha Matindi, alipotafutwa na Nipashe, alisema walikuwa katika hatua za mwisho za kisheria kumpata mtuhumiwa ili athibitishe kuwa mwanawe amefariki dunia kabla ya kukabidhi miili hiyo kwa ndugu.

Watu hao walifariki dunia wakipata matibabu Muhimbili baada ya kuungua kwa moto uliodaiwa ulitokana na gesi wakiwa nyumbani uliosababishwa na mmoja wa wanafamilia.

# Serikali yakazia msimamo shule za bweni

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetilia mkazo msimamo wake kuhusu shule za bweni na kusisitiza kwamba Waraka Namba 2 wa utoaji wa huduma ya kulaza bweni wanafunzi chini ya darasa la tano haujafutwa.

Taarifa ilitolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, baada ya kusambaa mtandaoni taarifa kwamba serikali imesitisha Waraka Namba 1 na Waraka Namba 2 ilizotoa awali.

Taarifa iliyosambaa mtandaoni ilikuwa na kichwa cha habari kwamba kikao cha TAMONGOSCO (Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania), TAPIE (Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Sekta ya Elimu) na serikali chafikia mwafaka mzuri kwamba nyaraka zote mbili zimesitishwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya serikali iliyotolewa jana, waraka huo ni msisitizo wa Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule wa mwaka 2020.

"Wadau wote wanapaswa kuzingatia waraka huu, hata hivyo, kama Waraka Namba 2 wa mwaka 2023 ulivyoelekeza, watakaoruhusiwa kupokea wanafunzi chini ya darasa la tano katika shule za bweni ni wale tu watakaopewa kibali maalum na Kamishna wa Elimu.

"Kwa hiyo wale wote waliokuwa na kibali cha Kamishna wa Elimu kwa sasa hawahusiki na katazo hili. Mchakato wa kuchambua suala hili na kuchukua uamuzi zaidi, utafanywa kwa kushirikisha kikamilifu wadau wote," alisema.

Pia taarifa hiyo imezungumzia kuhusu utekelezaji wa Waraka namba 1 wa mwaka 2023 wa Uboreshaji wa Huduma za magari na mabasi yanayotumika kusafirisha wanafunzi kwa kueleza kuwa nao uko pale pale.

Taarifa hiyo ikifafanua kwamba isipokuwa kwenye suala la kuajiri wahudumu wa mabasi wenye jinsia ya kike na kiume.

"Muda wa kuanza utekelezaji wa suala hili umesogezwa mbele kwa sasa, ili kupisha majadiliano na wadau na kupanga namna ya kutekeleza suala hilo la ajira za wahudumu wa magari na mabasi ya wanafunzi," ilisema taarifa hiyo.

Mwenyekiti wa TAMONGOSCO, Leonard Mao, alisema Jumatano wiki hii kuwa wadau wa elimu wengi wao kutoka sekta binafsi walikutana na viongozi wa Wizara ya Elimu wakiongozwa na Waziri Prof. Adolf Mkenda kujadili mambo mbalimbali ya sekta hiyo ikiwamo nyaraka zilizotolewa hivi karibuni.

Alisema baada ya majadiliano, serikali imesikiliza wadau wa elimu na hatimaye ikaona kuna makosa kupitia msingi wa maelezo waliyoyatoa wadau.

"Serikali imesikiliza wadau kwa moyo mkunjufu, kwa msingi wa maelezo yetu, serikali imeona ni vyema kusitisha hizi nyaraka, Waziri ametamka mbele yetu kwamba, Waraka Namba 2 wa mwaka 2023 umesitishwa na Waraka Namba 1 wa mwaka 2023 umesitishwa.

"Serikali imeona kuna makosa, imeona ni vyema kusitisha hizi nyaraka, kwa ujumla tumeshikana mkono, tumeipongeza serikali, wametuambia inaondoa hizi nyaraka tuendelee na ratiba mambo mengine yatarekebishwa polepole," alisema.



Wachuuzi wa mboga wakiwa wamejipumzisha, baada ya kukesha wakifanyabiashara, katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, alfajiri ya kuamkia jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mafuriko yatikisa, barabara zafungwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MVUA iliyonyesha kwa zaidi ya saa tano katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza, imesababisha mafuriko eneo la Mkuyuni, wilaya ya Nyamagana.

Pia imesababisha shughuli za usafiri kusitishwa kwa zaidi ya saa tatu, huku baadhi ya waendesha pikipiki wakinusurika kusombwa na mafuriko hayo.

Nipashe ilifika katika eneo la tukio na kushuhudia adha walizokuwa wakizipata wasafiri waliokuwa wakienda katika shughuli zao, huku wengine wakilazimika kuteremka kwenye daladala na kubebwa mgongoni na baadhi ya vijana waliowatoza Sh. 500 ili kuvushwa eneo hilo.

Kadhalika, askari wa usalama barabarani waliwahi katika eneo hilo na kuanza kutoa mwongozo kwa waendesha vyombo vya moto kwa kuwaelekeza maeneo salama ya kupita.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi waliokumbwa na adha hiyo, waliiomba serikali kujenga upya daraja hilo kutokana na kuwapo kwa mafuriko ya aina hiyo kila msimu wa mvua, ambayo yanaathiri makazi na maduka. Mmoja wa wakazi hao, Allan Abel alisema: "Hali hii imekuwa ya kila mwaka sasa mvua ikinyesha lazima maji yajae na hii inasababishwa na daraja hili kuwa finyu licha ya kuwa daraja linalounganisha barabara iendayo mikoani."

Anna Hamisi, mmoja wa wasafiri waliokuwa wakiwahi mabasi yaendayo mikoani alisema kutokana na kadhia hiyo alishindwa kusafiri kuelekea msibani ambako alikuwa akiwahi basi na muda wake wa kuondoka ukawa umepita.

Baadhi ya vijana waliokuwa wakiwavusha wananchi wakiwamo madereva pikipiki walisema kadhia hiyo kwao imekuwa baraka kutokana na baadhi yao kupata zaidi ya Sh. 15,000 kwa muda mfupi.

Mmoja wa madereva hao, Revocutus Shabani, alisema: "Kwa muda huu tu nimebeba zaidi ya watu 15 licha ya kuwa hali ya kuvuka daraja hilo haikuwa nzuri, tulikuwa tukisaidiwa na askari wa usalama barabarani."

Akizungumza kwa njia ya simu kuhusu utatuzi wa mafuriko katika daraja hilo, Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Paschal Ambrose, alisema daraja hilo si tatizo la mafuriko hayo. Alisema tatizo la mafuriko ni wananchi kutupa taka ovyo katika mitaro.

Alisema Halmashauri ya Jiji hilo inatakiwa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka ili kudhibiti vitendo hivyo.

# Waziri awa mbogo viongozi maslahi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeagizwa kuwachunguza baadhi ya viongozi wanaojihusisha na vitendo vya mgongano wa maslahi na kukinzana na wenzao hasa katika halmashauri nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akifungua mkutano wa baraza la wafanyakazi wa sekretarieti hiyo jijini hapa.

Alisema kwa kutumia mbinu za uchunguzi walizo nazo, wafuatilie kwa ukaribu viongozi wanaojihusisha na ukiukwaji wa maadili vikiwamo rushwa na mgongano wa maslahi na kwa wale watakaobainika kukengeuka misingi ya maadili na utawala bora, taratibu na sheria za nchi zichukue mkondo wake.

"Wako baadhi ya viongozi wa umma wanaojihusisha na vitendo vya mgongano wa maslahi wanapotimiza majukumu yao na wako wengine ambao wanakinzana na wenzao hasa katika halmashauri zetu. Kiongozi wa umma anapotoa kauli inayokinzana na kiongozi mwenzake au na mamlaka iliyomteua ni ukiukwaji wa maadili.

"Tabia na mwenendo huu si afya katika kuwaletea wananchi maendeleo endelevu na sio dhamira ya serikali. Hakikisheni viongozi wa umma wanazungumza lugha moja na kuheshimiana," alisema. Waziri Mhagama pia aliwakumbusha kutoa elimu kwa viongozi wa umma kuhusu matumizi sahihi ya madaraka.

"Waelimisheni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili umuhimu wa kiongozi kuwa mwaminifu anapotekeleza majukumu yake na athari zinazoweza kulipata taifa iwapo atashindwa kuwa mwaminifu na kujinufaisha yeye pamoja na watu wake wa karibu anapotekeleza majukumu yake," alisema.

# Wagonjwa 193 wachunguzwa viashiria ugonjwa Marburg

**Na Waandishi Wetu**

MGANGA Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, amesema watu 193 wakiwamo wahudumu wa afya 86, wanaendelea kuchunguzwa mkoani Kagera kutokana na kuchangamana na waathirika wa ugonjwa wa Marburg.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Prof. Nagu alisema serikali kupitia Wizara ya Afya Inaendelea kuwafuatilia watu hao.

"Bado tuna wagonjwa walioripotiwa wanane na watano kati yao walifariki dunia, watatu bado wanaendelea na matibabu na afya zao zinazidi kuimarika. Kikubwa wananchi waendelee kuonyesha ushirikiano katika kukabiliana na ugonjwa huu," alisema Prof. Nagu.

Katika hatua nyingine, mkoani Mwanza, nguvu kubwa imewekwa kwa wasafiri wanaotokea katika mkoa wa Kagera pamoja na wavuvi waishio visiwani kwa kuwataka kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya wataalam ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

Akizungumza na wadau mbalimbali katika kikosi kazi cha kukabiliana na maambukizi ya mlipuko wa ungojwa huo, Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma Mkoa wa Mwanza, Renard Mlyakado, alisema jamii inapaswa kuchukua tahadhari ya kutokushikana mikono na kuweka mazingira katika hali ya usafi.

"Tahadhari kubwa inahitajika ndani ya jamii kupitia viongozi wa dini na makundi mbalimbali yasaidie kufikisha elimu ya kutosha juu ya maambukizi ya ugonjwa wa Marburg unao ambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na binadamu kwenda kwa binadamu," alisema.

Msemaji wa Chama cha Wavuvi Tanzania (TAFU), Sijaona Karoli, alisema shida kubwa ya visiwani ni uhaba wa vituo vya afya na zahanati, hivyo waliomba serikali iweke vituo vya dharura ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Thomas Rutachunzimbwa, alisema wamejipanga kukabiliana na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kufahamu maana ya ugonjwa, namna unavyoenezwa, dalili zake na njia za kujikinga.

Baadhi ya wananchi wameiomba serikali kuendelea kutoa elimu ya kukabiliana na ugonjwa huo ili usije kuenea katika maeneo zaidi, huku wakiahidi kuendelea kutoa ushirikiano pindi watakapo kutana na watu wanaoshukiwa. Mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi, Awadhi Adam, alisema wanaendelea kusubiri elimu kutoka kwa serikali ambayo itawaongoza kujilinda na ugonjwa huo ili usisambae na kuongeza vifo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Isesanda Kaniki, alisema wameunda timu ya utoaji elimu kwa jamii na ufuatiliaji wa haraka wa tiba kwa mgonjwa anaeashiria kuwa na dalili.

**Imeandaliwa na Restuta Damian (BUKOBA), Rose Jacob (MWANZA) na Titus Mwombeki (KAGERA).**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
25.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe 28-03-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 460 DYG/ T 879 EAU T 681 DUB / T 881 EAU T 188 DFC / T 568 EAZ T 973 DTN / T 572 EAZ**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 25.00**
   **Upana - mita 5.10**
   **Kimo - mita 5.60**
3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217340702

# Mgombea wa urais TLS atishia kukata rufani kwa kuenguliwa

**Na Grace Gurisha**

SAKATA la uchaguzi wa kugombea urais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), limeanza kushika kasi baada ya mtia nia wa nafasi hiyo, Sweetbert Nkuba, kutishia kukata rufani kupinga kuondolewa kwa jina lake kwa madai kuwa yeye ni mtumishi wa serikali.

Mei, mwaka huu, TLS inatarajia kufanya uchaguzi wa kumpata rais, baada ya Prof. Edward Hosea kumaliza muda wake wa kipindi cha miaka miwili ya kuongoza chama hicho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, jijini Dar es Salaam, Nkuba alisema hajakubaliana na uamuzi wa kuondolewa jina lake uliotangazwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Charles Rwechungura.

"Nalaani kitendo hiki cha kuenguliwa kwa jina langu kwenye hatua za awali za mchakato wa uchaguzi huu kwa sababu ambazo si za kweli licha ya kwamba nilijieleza kutokana na pingamizi lililowasilishwa juu yangu," alisema Nkuba.

Pia alisema anataka kufanya hivyo ili haki ionekane inatendeka, lakini pia kuhakikisha uwapo wa demokrasia kwenye vyama vyote vya kitaaluma ili kitendo hicho kisijitokeze tena katika uchaguzi mwingine.

Nkuba alisema kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi za TLS, ana sifa za kugombea na kwamba kulikuwa na hoja mbili, moja hakuwahi kufanya kazi ya uwakili kwa miaka 10 na pili kuwa yeye ni mtumishi wa serikali.

"Sababu hizo sijakubaliana nazo kwani tangu nimeapishwa kuwa wakili huu ni mwaka wa 13 au 14 ni zaidi ya miaka 10 na kuhusu kuwa mtumishi wa serikali, nilishaacha kazi serikalini kwa kufuata taratibu zote za kisheria kwa hiyo kamati imetumia maneno ya fununu kutoa uamuzi.

"Sitaki kueleza sababu kiundani kwa kuwa nina jopo la mawakili walionipendekeza kuwania urais wakiongozwa na Jeremiah Mtobesya, hivyo jopo linafanya utaratibu wa kukata rufani kwa sababu ninazo sifa za kuwa mgombea nimeshangazwa na kitendo cha kuenguliwa kwa jina langu," alisema Nkuba.

Mmoja wa mawakili wa Nkuba, Dk. Aloys Rugazia, alisema rufani hiyo wataikata mbele ya Kamati ya Rufani ya TLS kwa sababu kigezo kilichotumika kumng'oa mteja wake ni cha kibaguzi kwakua kufanya kazi serikalini haiwezi ikamtia Wakili dosari kiasi hicho.

Dk. Rugazia alisema lengo ni kupata tafsiri ya kufanya kazi ya uwakili kwa kipindi cha miaka 10 kuna hesabiwa kwa kigezo kipi.

"Kama rufani hii ikienda tofauti na matakwa ya mteja wangu, tutalazimika kutoka kwenda Mahakama Kuu kukata rufani na pia nina imani kuwa kamati ya rufani ya TLS ikiongozwa vyema itatoa uamuzi wa haki," alisema Dk. Rugazia

## Machinjio yafungwa kisa kukithiri uchafu

**Na Idda Mushi,** MIKUMI

BODI ya Nyama Tanzania imefungia kutoa huduma machinjio ya Mikumi katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Mikumi, Kilosa mkoani Morogoro kutokana na kukithiri kwa uchafu, hivyo kuhatarisha afya za walaji.

Licha ya kuchukua hatua hiyo, Bodi ya Nyama Tanzania kupitia Ofisa Ukaguzi Geofrey Kakuru, imemwelekeza mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kuhakikisha machinjio hayo yanafanyiwa ukarabati kwa wakati ili kukidhi vigezo vilivyowekwa na mamlaka husika ili kulinda afya za walaji wa nyama.

Hatua hiyo imechukuliwa na bodi baada ya machinjio hayo kubainika kuwa na changamoto mbalimbali ikiwamo miundombinu mibovu ya utoaji majitaka na taka ngumu na sakafu iliyoharibika.

Tatizo lingine ni machinjio hayo kukosa uzio, kuwa na nyenzo chakavu za utendaji kazi, vyoo visivyo na ubora unaotakiwa na kukosekana banda maalum la kuhifadhia ngozi, hivyo kusababisha ngozi kuanikwa kwenye udongo.

Mengine ni mkanganyiko wa ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi wa machinjio hayo hali inayosababisha malimbikizo ya madai ya mishahara kwa wafanyakazi ambayo imekuwa hailipwi kwa wakati.

Wakizungumza baada ya kufungwa kwa machinjio hayo, Katibu wa Machinjio, Raphael Kizinzili na mjumbe Alfred Mtulila walikiri kuwa awali serikali ilitoa Sh. milioni 11 kwa ajili ya kufanya marekebisho ya miundombinu lakini imechukua muda mrefu hadi sasa bila kufanyika.

"Hali hii imezua hali ya sintofahamu kwa fedha hizo za benki kwani pia zimeendelea kupungua na haijulikani zinafanyia nini kwani machinjio yameshindwa kukarabatiwa," alisema Kazinzili.

Mbali na machinjio ya Mikumi kuwa tegemeo kwa wakazi na wafanyabiashara wengi wa nyama wa mamlaka ya mji mdogo wa Mikumi kwa ajili ya kitoweo na biashara, pia yamekuwa chanzo cha mapato katika kuchangia maendeleo ya mji huo.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Profil Masawe 'Mr UK', akipandisha bendera ya CCM, baada ya kuzindua shina la wakereketwa la Wazazi tawi la Wazo, wakati wa ziara ya Kamati ya Utekelezaji ya Wazazi wilaya, kukagua uhai wa jumuiya katika Kata ya Wazo, hivi karibuni. Wa (pili kushoto) ni Mwenyekiti wa Wazazi wa Kata hiyo, Jesca Mrope na (kulia) ni Katibu wa Wazazi wa Wilaya hiyo, Daima Utanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Zimamoto Bara yataka iunganishwe Zanzibar

**Na Restuta James**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limeomba liunganishwe na kikosi cha Zanzibar ili kuunganisha rasilimali watu, vifaa na utaalam baina yao.

Aidha, limependekeza sheria inayounda Jeshi hilo ya mwaka 2007 sura ya 427, ifanyiwe marekebisho ili kuongeza kamisheni ya uokoaji kwa kuwa haijatengewa nafasi inavyostahili ndani ya sheria.

Mapendekezo hayo yaliwasilishwa na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, alipowasilisha maoni mbele ya Tume ya Kurekebisha Mifumo ya Haki Jinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Chande.

Alisema vikosi hivyo vya Tanzania Bara na Zanzibar, vikiunganishwa vitaongeza tija na ufanisi wa kazi.

Kamishna Jenerali Masunga alisema wamewasilisha mambo mengi kwenye tume hiyo ikiwamo muundo wa jeshi, ajira, changamoto na mapendekezo ya kuliboresha.

Kuhusu vitendea kazi, alisema haviridhishi na kuongeza kuwa serikali imeshaanza kushughulikia tatizo hilo.

"Tuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi. Kwa upande mwingine tunaishukuru sana serikali kwamba katika hili tayari hatua zimeshachukuliwa kuhakikisha kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linapata vitendea kazi vya kisasa na vya kutosha," alisema.

Jenerali Masunga pia alisema hatua hizo zitaliwezesha jeshi hilo kuwa na vifaa vya kutosha katika kipindi cha ndani ya muda mfupi. Alisema mikakati iliyopo ni kuhakikisha Jeshi hilo linatoa huduma zake wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2025.

Katibu Mtendaji wa Chama cha Madini Tanzania (TCM), Mhandisi Benjamin Mchwampaka, alisema wameainisha maboresho kwenye sheria na kanuni ikiwamo adhabu ya faini ya hadi Sh. bilioni 10, inayotozwa kwenye kampuni ya madini inayoshindwa kuwasilisha taarifa kwa wakati.




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Amref, Dk. Florence Temu (kulia) kuhusu miradi ya kifua kikuu inayotekelezwa na shirika hilo nchini, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kifua kikuu Duniani, yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Japan yaisaidia WFP bil. 2.1/- kununua chakula kwa wakulima

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) litatumia Sh. bilioni 2.1 walizosaidiwa na serikali ya Japan kununua mazao kwa wakulima wazawa kwa ajili ya chakula cha kulisha wakimbizi katika kambi za Nyarugusu na Nduta mkoani Kigoma.

Hatua hiyo inakuja baada ya serikali ya Japan kupitia ubalozi wake nchini Tanzania jana kutoa msaada wa Dola za Kimarekani 900,000 kwa ajili kuisaidia WFP kununua chakula cha wakimbizi 200,000 walioko kwenye kambi hizo.

Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa, alisema fedha hizo zimetolewa ili kuisaidia WFP kukidhi mahitaji ya chakula na lishe kwa wakimbizi nchini Tanzania hususani katika kambi hizo mbili.

Aidha, Mwakilishi Mkazi na Mkurugenzi wa WFP Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, alisema Tanzania ina zaidi ya wakimbizi 200,000 kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, hivyo msaada huo umetolewa kipindi sahihi wakati WFP ikiwa na upungufu wa fedha za kununulia chakula.

"Tunawashukuru sana wenzetu wa serikali ya Japan kwa msaada huu. WFP tunaamini msaada huu utaleta mabadiliko katika maisha ya wakimbizi nchini Tanzania," alisema.

Kuhusu matumizi ya fedha hizo, mkuu huyo wa WFP alisema fedha hizo zitatumika kununua mazao kwa ajili ya chakula kutoka kwa wakulima wa ndani kutoka mkoa wa Kigoma na mikoa mingine inayozalisha mazao ya chakula kwa wingi.

"Mazao yote kuanzia ya nafaka, kunde, maharage, mafuta ya kupikia na chumvi vyote vitanunuliwa kutoka kwa wakulima wa hapa nchini," alisema.

Alisema lengo ni kununua mazao hayo hapa nchini na kuwainua wakulima wa ndani kuwaendeleza kwenye kilimo chao.

"Hii ni fursa kwa wakulima wa hapa nchini, watapata soko la uhakika la mazao hayo yanayohitajika kwa ajili ya kulisha wakimbizi waliopo mkoani Kigoma katika kambi za Nyarugusu na Nduta," alisema.

# Makandarasi wazawa walilia sheria ya dhamana ya malipo

**Na Romana Mallya**

MAKANDARASI wazawa wameishauri serikali itunge Sheria ya Dhamana ya Malipo itakayolinda kazi wanazozifanya, badala ya kufanya shughuli zao kwa kutumia mikataba ambayo wakati mwingine huwaumiza.

Mwenyekiti wa kamati ya mpito ya uanzishaji wa Chama cha Umoja wa Makandarasi Tanzania (TUCASA), Samweli Marwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano uliokwenda sambamba na kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi.

Alisema: "Hii ndiyo shida kubwa tunayopata makandarasi baadhi ya nchi zetu, shida ni kwamba unapoingia mkataba, anayekupa kazi anakwambia ulete performance guarantee (ufanisi wa kazi) kwa maana kwamba usipofanya kazi vizuri ana mahali anaweza kuchukua hasara zake".

Aliongeza: "Lakini, sisi hatuna kitu kinaitwa dhamana ya malipo wakati nchi nyingine wanayo ili ikupe uhakika kwa kuwa kazi ya ujenzi hatuuzi nyumba, barabara wala madaraja, sisi tunauza ujuzi wa kutengeneza nyumba anayejenga ni mwenye nyumba au barabara".

Marwa alisema kwa namna biashara ya makandarasi ilivyo ni lazima anunue vifaa ili kufanya kazi na ndipo baadaye mhusika amrejeshee fedha alizotumia.

"Anapochelewa kurejesha wakati mwingine wanakuambia kwamba, wewe si ulisema una fedha, ndiyo nilisema nina fedha lakini, siyo fedha ya kujengea barabara yako ni fedha zangu, kama ninaitumia ni lazima tuwe na maelewano, ninapokukopesha basi unipe riba.

Marwa alisema kupitia umoja huo, utawawezesha kuorodhesha baadhi ya sheria ambazo zina mapungufu yakiwamo malakamiko hayo ya dhamana ya malipo ili serikali iwe nayo.

Mjumbe wa kamati ya mpito ya uanzishaji wa TUCASA, Vivian Ibrahimu akizungumzia kuhusu makandarasi wanawake, alisema ndani ya chama hicho kutakuwa na kamati maalum ambayo itakuwa inapeleka masuala ya kundi hilo.

"Asilimia 30 ambayo inasemwa serikalini ambayo mama ametupa wanawake makandarasi kuwa tupewe miradi inayotolewa na serikali, bado tunaisimamia na kuipambania ili tuione kikamilifu kwa sababu kwenye utekelezaji mara nyingine unahitaji kanuni na sheria," alisema.

Alisema bado wanaendelea kufuatilia ili asilimia hizo waione kwenye utendaji halisi kwa makandarasi wanawake.

Vivian alisema ushiriki wa makandarasi wanawake kwenye miradi bado hawajafikia asilimia 30 ambayo serikali inataka wapewe.

Alisema: "Zipo taasisi ambazo zinatoa kazi kwa wanawake lakini hazifiki asilimia 30, ninafikiri kwamba ikiwa ni sheria inatekelezeka lakini kwa sababu ni tamko halijawa sheria, tunaamini TUCASA itasaidia kwa kuwa tupo ndani yake".

# China yaahidi kuisaidia Tanzania sekta ya afya, ulinzi na usalama

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI ya China imesema itaendelea kuiunga mkono Tanzania kwenye mambo mbalimbali ikiwamo masuala ya afya, ulinzi na usalama.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 10 tangu Rais wao, Xi Jinping alipofanya ziara nchini mwaka 2013.

Alisema ujio wa Xi Jinping ulichangia mambo mengi Tanzania ikiwamo kubadilisha taswira na muonekano kwenye nyanja mbalimbali.

"Kupitia ziara hiyo Tanzania na China tumeongeza ushirikiano kwenye utamaduni, elimu, afya, uhusiano wa kijamii, biashara, pamoja na kuchangia maendeleo mbalimbali kwenye jamii ya watu wakiafrika," alisema.

Balozi Mingjian alisema nchi hizo zimefanikiwa kusaidiana kwenye mambo mengi ya kimataifa ikiwamo yale ya haki na uadilifu.

"Ziara ilitusaidia kutatua kwa pamoja vikwazo vilivyokuwapo, kuongeza umoja na mshikamano kwa sababu urafiki wetu ulianza tangu kipindi cha Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere".

Aliongeza kuwa ziara hiyo pia imesababisha kukua kwa kibiashara kwa asilimia 23.7 kwa mwaka hali iliyosababisha nchi hizo kutengeza Dola bilioni 83.1 kwa mwaka.

"Pia ilifanikisha kujengwa kwa maktaba kubwa kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Mafunzo na Ufundi Kagera, ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambao unaendelea, pamoja na Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa alisema ujio wa Rais wa China mwaka 2013 ulijikita kwenye mambo manne ikiwamo amani, msamaha, uaminifu pamoja na kushirikiana kwenye mambo mema na mazuri.

Kawawa alisema: "Kwa kipindi chote hicho China imekuwa mwekezaji mzuri kupitia takwimu za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), China ina miradi mingi hapa nchini, ambayo imesaidia kutoa ajira kwa vijana wa mtaani zaidi ya 300,000".

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Rais Samia kuwaita mashabiki kuishangilia Stars

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kuwakaribisha wapinzani wao Uganda (Cranes), katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mashindano hayo ambayo fainali zake zitafanyika Februari, mwakani huko Ivory Coast na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Taifa Stars iko Kundi F pamoja na nchi za Algeria, Niger na Uganda.

Algeria juzi ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Niger na kufikisha pointi tisa, zinazowapa uongozi kwenye kundi hilo.

Katika kuhakikisha Taifa Stars inafuzu fainali hizo za AFCON kwa mara ya tatu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuipatia timu hiyo zawadi ya Sh. milioni 500.

Rais Samia amefanya hivyo, wakati bado anaendelea na hamasa yake ya kununua mabao yanayofungwa na Simba na Yanga ambazo zinashiriki mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na CAF.

Lakini katika kufahamu mbali na Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche na benchi la ufundi kufanya maandalizi yake vizuri ya kusaka ushindi, ameahidi kutoa tiketi 4,000 kwa mashabiki ili waingie uwanjani kuwashangilia vijana wake ambao wanapeperusha bendera ya Tanzania.

Mbali na Rais Samia, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, klabu za Simba, Yanga, Azam FC na wadau wengine nao wameonyesha kumuunga mkono kiongozi huyo namba moja nchini kukata tiketi na kufanya idadi ya mashabiki watakaopata kufikia kuzidi ya 10,000.

Tunampongeza Rais Samia kwa kuchukua uamuzi huo kwa sababu inafahamika shabiki ni mchezaji wa 13 ambaye ana nafasi muhimu katika kuhamasisha timu kupata ushindi na hatimaye kufikia malengo.

Ni vizuri Taifa Stars inapocheza kwenye uwanja wa nyumbani, mashabiki wake wakajitokeza kwa wingi kuishangilia kwa sababu kufanya hivyo kunawaongezea nguvu ya kupambana na hatimaye kupata matokeo chanya.

Ni jambo lisilojificha kama Simba na Yanga wanapokuwa na mechi zao za kimataifa au matamasha ya Simba Day na Siku ya Mwananchi, mashabiki hufurika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakiwa na shangwe kabla na wakati wa mchezo. Na huendeleza furaha pale timu zao zinapovuna matokeo chanya, basi jambo hilo linatakiwa kuonekana kwa wingi ule ule Jumanne wakati Stars itakapowakaribisha Uganda.

Haitajalisha kama shabiki atavaa jezi au la, lakini suala la kuhudhuria katika mchezo huo ni muhimu kwa sababu mbali na kuendeleza kampeni za kufuzu fainali za AFCON, lakini ushindi au matokeo ya sare yataifanya Tanzania kupanda kwenye viwango vya ubora vinavyotolewa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Huu ni wakati wa kuonyesha mapinduzi kwenye mchezo wa soka, mashabiki kujitokeza uwanjani kuipa sapoti Stars ni uamuzi rafiki kama ambavyo kocha mpya wa timu hiyo alivyosema baada ya kutambulishwa kubeba mikoba iliyoachwa na Kim Poulsen.

Tunafahamu hakuna kisichowezekana, ni suala la viongozi wa matawi kuhamishia nguvu zao wanazozitumia wakati timu zao pendwa zinapokabiliwa na mechi za kimataifa kuwahamasisha wanachama na mashabiki kujitokeza uwanjani na kuishangilia Stars ambayo ni ya Watanzania wote.

Kama uwanja huo ulijaa wakati wa mechi ya ufunguzi au katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Timu ya Taifa ya Brazil uliochezwa mwaka 2010, siku chache kabla kikosi hicho hakijaelekea Afrika Kusini kwenye fainali za Kombe la Dunia, hata sasa mashabiki wanaweza kufanya hivyo na kufungua ukurasa mpya kwa Stars.

Mungu ibariki Taifa Stars katika kampeni hii ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za AFCON.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga si tegemeo kuzalisha wachezaji Stars

**KAMA** kawaida ya Watanzania, mara baada ya kutangazwa majina ya wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), hakukukosekana maneno.

Wengine walionekana kukubaliana na kikosi kilichotajwa, lakini baadhi walionekana kuwa na mashaka na timu hiyo.

Kuna baadhi ya mashabiki wa Stars wao ni mashabiki tu wa wachezaji fulani, asipoitwa tu katika kikosi kwao ni nongwa.

Kikosi cha wachezaji 31 kiliitwa huku 19 kati ya hao wanacheza soka la ndani kwenye klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara na wanaobaki wanacheza nje ya nchi.

Kutokana na sababu za mazoea au kukariri, wapo watu walioanza kuhoji ni kwa nini Simba na Yanga zina wachezaji wengi wa kigeni, kiasi hata Watanzania wanaochaguliwa kutoka timu hizo sio wale tegemeo sana kwenye klabu hizo?

Baadhi wakaenda mbali na kusema ikiwezekana basi idadi ya wachezaji wageni ipunguzwe ili kuwapa nafasi nyota wazawa kwa ajili ya kupatikana kwa Taifa Stars imara. Inashangaza kuona hata baadhi ya wachambuzi wanakuwa na mawazo haya kwenye karne hii ambapo soka ni biashara na si la ridhaa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Wakati wanaongea hivyo, kikosi cha Senegal kikatajwa, ambapo wachezaji wote walioitwa wanacheza soka la kulipwa Ulaya, isipokuwa Pape Sakho tu pekee ambaye ametoka Afrika, katika klabu ya Simba.

Hapo utaona hakuna mchezaji yeyote wa Senegal aliyechaguliwa kutoka nchini mwao, na kwenye bara la Afrika ni mmoja tu, ambaye ni Sakho.

Simba au Yanga ni kitu kingine kabisa na timu ya taifa ni kitu kingine vile vile. Kama Senegal haikuita wachezaji kutoka Simba na Yanga za Senegal na ikawa ya taifa, si vibaya siku ikaitwa Stars ambayo haina mchezaji anayeichezea kwa vigogo hao na ikashinda na mambo yakaendelea tu.

Kuna kitu ambacho Watanzania tunakikosa na ili kusaka tatizo tunakimbilia kuona wachezaji kutoka nje ya nchi ni tatizo.

Kwanza kabisa nataka niseme Simba na Yanga ni klabu zinazojitegemea na zinahitaji wachezaji bora kutoka sehemu yoyote ile duniani ili kupata mafanikio au kutwaa mataji na wala si vitalu vya ajili ya wachezaji wa timu ya taifa.

Wachezaji bora na wenye viwango vya juu wa Stars hata siku moja hawatotokana na kuwapunguza wachezaji ili wao wapate nafasi. Tuziache Simba na Yanga ziendelee na mipango yake kwa sababu uwepo wa wachezaji wa kigeni katika klabu hizo ndiyo kwa kiasi kikubwa zimefika hapo zilipo kwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano kimataifa. Simba ambayo kwa miaka mitano, imetinga mara tatu Ligi ya Mabingwa Afrika na mara moja Kombe la Shirikisho kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kuwapo kwa wachezaji wa kigeni.

Sipati picha kama kwenye michuano hii, Simba na Yanga zingekuwa na wachezaji wa Kibongo, hasa hawa wa sasa kama zingeweza kufika zilipofika.

Mfano mdogo, mpaka sasa mabao yaliyofungwa na timu hizo, ambapo kila bao inatolewa Sh. milioni tano na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, mabao yote yamefungwa na wachezaji wa kigeni, kasoro moja tu ambalo lilifungwa na Mudathir Yahaya wa Yanga katika mechi dhidi ya TP Mazembe, ikishinda magoli 3-1.

Vile vile hata huko nyuma ambako timu zetu zilikuwa hazina idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni, bado ilikuwa haifanyi vyema.

Tusikimbie tatizo la msingi kama Watanzania. Kwanza kabisa tuangalie namna gani ya kuzalisha wachezaji ambao watakuja si wachezaji tu peke yake bali wapambanaji. Halafu wawe na utamaduni wa kutoka kwenye kucheza soka la kulipwa, ili siku Stars ikitangazwa, robo tatu watoke nje. Vile vile angalau sasa serikali ianze kuangalia suala la uraia pacha hasa kwa wanamichezo, nayo inaweza kusaidia pia kurahisisha kuwapata wachezaji wengi wenye asili ya Kitanzania. Tukifika hapa, tutaacha kutaka kuzifanya Simba na Yanga kuwa vitalu vya Stars, kwani hatutokuwa na ulazima wa kutaka wawe na wachezaji wengi wa Kitanzania ili kuipata Stars bora.

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa taasisi ya Don Bosco Tech Africa Padre, George Tharaniyil (wa pili kushoto), akikabidhi muongozo wa kuratibu huduma bora za mafunzo na kazi kwa Padre Innocent Bizimana kutoka Don Bosco Madagascar katika mkutano mkuu wa mwaka wa wadau, jijini Dar es Salaam jana. Kauli mbiu ya mkutano huo, ilikuwa ni kuboresha elimu ya ufundi ili kufanikisha upatikanaji wa ajira na maisha bora ya vijana wa Afrika. Wengine ni Mfadhili wa Don Bosco kutoka Ujerumani, Steffen Mohlendick (kushoto) na Padre Jose Lorberth kutoka Don Bosco Makao Makuu, Roma nchini Italia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati ya Bunge yapitisha makadirio ya uwekezaji, viwanda, biashara 2023/24

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imepokea na kupitisha makadirio ya matumizi na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zake.

Aidha, kamati hiyo imeishauri serikali kuongeza wigo wa bajeti kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara hususani katika utafiti wa viwanda, utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania na uendelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo ili kutekeleza majukumu yake na kuendana na maendeleo yanayofanyika katika sekta zinazozalisha malighafi za viwandani. Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Kihenzile, alisema hayo jana wakati Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ikiwasilisha taarifa ya makadirio ya matumizi na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/24 katika ukumbi wa Bunge jijini Dodoma.

Wajumbe wa Kamati hiyo walitoa maoni mbalimbali yaliyolenga kuboresha na kuwezesha uendelezaji wa sekta hiyo inayofungamanisha sekta zote za uzalishaji kwa ufanisi ili kuongeza ajira, pato la taifa na kuleta maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi nchini.

Akiwakilisha taarifa ya makadirio hayo, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk Ashatu Kijaji, aliomba kutengewa Sh. 117,817,998,000 kwa mwaka 2023/24. Kati ya fedha hizo, Sh. 74,251,494,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi 43,566,504,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, Dk. Kijaji aliihakikishia kamati hiyo kuwa wizara itatekeleza maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa ili kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na kutimiza azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi shindani wa viwanda na utafutaji wa masoko ya ndani na nje kwa mazao na bidhaa za Tanzania.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, alisema wizara imeweka malengo na mikakati mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2023/24 inayolenga kuendeleza sekta za uwekezaji, viwanda na biashara kwa kushirikiana na sekta fungamanishi zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, madini, uchukuzi na ujenzi.

# Viongozi AMCOS wadaiwa kuiba pembejeo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

VIONGOZI wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) mkoani Shinyanga, wamedaiwa kujihusisha na wizi wa pembejeo hasa viuatilifu na vinyunyizi vya kuulia wadudu.

Licha ya serikali kuboresha sekta ya kilimo, imeelezwa kuwa bado kumekuwa na tatizo kwenye usambazaji wa viuatilifu vya kuulia wadudu na vinyunyizi kwa wakulima na kwamba viongozi wa AMCOS ndio wamekuwa wakijihusisha na wizi wa pembejeo za wakulima.

Hayo yalibainishwa juzi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Usambazaji wa Viuatilifu vya Pamba, Protas Henry, kwenye kikao cha Bodi ya Pamba Tanzania na waandishi wa habari.

"Katika usambazaji wa viuatilifu vya kuulia wadudu na vinyunyizi, tumekuwa tukikabiliwa na tatizo la wizi wa pembejeo hizi wakihusika na viongozi wa AMCOS, pamoja na viongozi wa kisiasa kuingilia ugawaji wa viuadudu na vinyunyizi na kuharibu utaratibu wakiwamo na maofisa ugani na watendaji wa vijiji.

"Viongozi hao pia wamekuwa wakighushi taarifa za kwenye fomu za kugawia viuadudu na vinyunyizi au kutojaza kabisa kwa lengo la kutengeneza mianya ya wizi wa pembejeo," alisema.

Kutokana na baadhi ya viongozi wa AMCOS kudaiwa kujihusisha na wizi huo, majalada 12 yameshafunguliwa katika vituo vya polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya uchunguzi na kesi sita zimeshafunguliwa mahakamani na moja tayari imetolewa hukumu na mhusika alilipa faini ya Sh. milioni moja.

Katika hatua nyingine, Henry aliwakumbusha viongozi wa AMCOS na watendaji wengine waliopewa dhamana ya kusambaza na kugawa viuatilifu vya kuulia wadudu na vinyunyizi kwa wakulima kutimiza wajibu wao kusaidia wakulima na kujiepusha na vitendo vya wizi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, James Shimbe, alisema ndani ya utawala wa miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, bodi hiyo inajivunia mafanikio makubwa ikiwamo kulinyanyua tena zao la pamba ambalo lilitoka katika hatari ya kufa.

Alisema pamba kwa sasa inakwenda vizuri na katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/23 wanatarajia kupata mavuno ya zaidi ya tani 500,000.

# GGML na halmashauri zaingia mkataba bil. 19/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imesaini mkataba wa makubaliano wa Sh. bilioni 19 na Halmashauri ya Mji Geita, Wilaya ya Geita pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Bukombe pamoja na Mbogwe.

Makubaliano hayo yametiwa saini juzi mjini Geita na kushuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela pamoja na wakuu wa wilaya za mkoa huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji GGML, Elder Damon alisema kutiwa saini kwa makubaliano hayo ni kutekeleza mpango wa uwajibikaji kwa jamii kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema Sh. bilioni 9.8 zimetengwa kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Geita na kwamba kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, imetengewa Sh. bilioni 8.6.

Damon alisema katika makubaliano hayo GGML pia itatoa Sh. milioni 600 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa halmashauri tatu za Mbogwe, Chato na Bukombe mkoani Geita, kwamba kila moja itapata Sh.milioni 200.

Alisema mpango wa CSR wa mwaka huu ni mwendelezo wa mipango ya awali unaolenga kujumuisha maendeleo yaliyofikiwa na GGML, hadi sasa katika maeneo ya mazingira, miundombinu, afya, elimu na biashara katika jamii.

"Binafsi inanipa furaha kushuhudia matokeo ya miradi yenye mafanikio katika maisha ya Watanzania, hasa wale wanaoishi karibu na mgodi. GGML inajitahidi kuunga mkono matarajio ya Serikali ya Tanzania ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi katika jamii zinazowapokea.

Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo alisema watu wengi hawafahamu kwamba kabla ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kufanyiwa marekebisho mwaka 2017, tayari GGML ilikuwa inatekeleza mpango wa CSR kwa kutoa Sh. bilioni tisa kugharamia miradi mbalimbali ya kijamii mkoani Geita.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela, alisema: "Nichukue fursa hii kuipongeza GGML kwa kuwa kinara wa uchimbaji endelevu wa madini. Nawashukuru pia kwa kuwa na subira na uungwana wa kutuvumilia kukamilisha mchakato wa utiliaji saini hii ya makubaliano ambao umekuwa ukisogezwa mbele mara kwa mara".

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wa Geita kuchangamkia fursa za miradi hiyo kwa kuhakikisha mahitaji ya makandarasi yanapatikana ndani ya mkoa huo.

Pia aliagiza viongozi wa halmashauri kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi ili kutoacha upungufu wowote.

# ATE yashauri programu za ujuzi kuinua wanawake

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimesema ili kuongeza usawa wa kijinsia mahali pa kazi na wanawake kushika nafasi za juu za uamuzi, ni vizuri kampuni zikawekeza katika programu zitakazoliongezea ujuzi kundi hilo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati chama hicho kikizindua awamu ya tisa ya programu ya mwanamke na uongozi yenye washiriki 73 kutoka kampuni 22, huku mwaka jana idadi yake ikiwa ni 65.

Alisema programu hiyo ilianza mwaka 2016 baada ya kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye wakati huo alikuwa ni Makamu wa Rais.

"Lengo ni kuongeza usawa wa kijinsia katika maeneo yetu ya kazi na wanawake waweze kushika nafasi mbalimbali ziwe za juu, katikati hata kwenye bodi, hili kwetu ni jambo sahihi.

"Hivyo, ni vizuri kampuni zikawekeza, siyo tu kwenye programu ya mwanamke kiongozi, lakini pia katika programu mbalimbali na kuwaongezea wanawake ujuzi katika maeneo mbalimbali, ili waweze kutoka katika nafasi moja kwenda nyingine," alisema Doran.

Doran alisema ATE inatoa mafunzo hayo kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wanawake katika maeneo matatu ambayo ni uongozi, mawasiliano na uendeshaji wa bodi.

Mkurugenzi Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, Godfrey Rutasingwa alisema benki hiyo imetoa wanawake 16 mwaka huu ambao wamejiunga na mafunzo hayo.

Alisema benki yao inaamini katika nguvu ya wanawake na katika kufanya hivyo, wamekuwa wakiwekeza kila mwaka kuwaendeleza wafanyakazi wao ili wakue na kushika nyadhifa tofauti za uongozi.

Rutasingwa alishauri kampuni nyingine zitenge sehemu za rasilimali zao kuendeleza wafanyakazi wanawake kwa kuwa waliopiga hatua kwenye hilo eneo wanaona manufaa makubwa kupitia michango yao na uwakilishi wao kwenye ngazi ya uamuzi.

Alisema kabla ya kuleta washiriki wanawake kwenye programu hiyo walikuwa wanaendesha programu zao za ndani kwa kundi hilo.

Makamu wa Rais wa Kampuni ya Geita Gold Mine (GGM), Simon Shayo alisema wamekuwa wakileta washiriki tangu kuanza kwa programu hiyo na mwaka huu imewatoa washiriki watano.

Msimamizi wa Miradi kutoka Kampuni ya Kuhifadhi Mafuta Tanzania (TIPER), Halima Kidula alisema ameamua kushiriki programu hiyo ili kuboresha na kuongeza ufanisi katika uongozi na kusaidia wengine kwenye taasisi yake.

Mtaalam wa Mawasiliano na Matangazo, Maureen Njeri, alisema ameamua kushiriki programu hiyo ili kujifunza na kuwa kiongozi bora mwanamke.




Mkuu wa Wilaya ya Kipolisi Kawe SP Deus Shatta (kushoto), akipokea msaada wa viakisimwanga 'Reflectors' kutoka kwa Mkuu wa kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet Tanzania, Matina Nkurlu mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwasaidia kwenye utendaji kazi wao katika kuadhimisha wiki ya nenda kwa usalama barabarani. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Kawe ASP Rose Maira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi maji pembezoni mbioni kukamilika

**Na Joseph Mwendapole**

UTEKELEZAJI wa mradi wa kusambaza maji safi nje ya mtandao unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) umeendelea kushika kasi katika hatua mbalimbali na hadi sasa umefikia asilimia 90.

Utekelezaji wa mradi huo unalenga kuhudumia wananchi 150,388 wa mitaa ya Feri, Upendo, Tungi, Magogoni (Manispaa ya Kigamboni), Mwanamtoti/Butiama, Mianzini, Dovya, Mwembebamia, Kisewe/Magengeni (Manispaa ya Temeke) na Mgeule/Mgeule Juu (Ilala).

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Msimamizi wa Mradi Mhandisi Stephen Urio, alisema utekelezaji unahusisha miradi tisa itakayohudumia wakazi wa mitaa 13 katika manispaa za Kigamboni, Ilala na Temeke. Alisema kuwa mradi unahusisha ulazaji wa bomba la inchi 14 hadi 2.5 kwa umbali wa kilomita 138.45 na kuunganisha zaidi ya wateja 2,000 wa majumbani. "Mradi unatekelezwa na mkandarasi M/S Ceytun - Kasco Joint Venture kwa thamani ya Sh. bilioni 10.8," alisema Mhandisi Urio.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Upendo, Zacharia Mkundi, aliishukuru serikali kwa utekelezaji wa mradi huo ambao umepita katika mtaa wake.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia maji ya chumvi na yenye gharama kubwa kutoka kwa watu binafsi, hivyo anafurahi kwa kuwa wakazi wa upendo wanaenda kupata majisafi na salama kutoka DAWASA. "Kwanza nipende kuishukuru serikali kwa hiki kinachoendelea katika mtaa wangu kwani sasa muda umewadia kwa wakazi wa Upendo kufurahia huduma ya maji safi na salama kwa kuwa kwao kilikuwa kitendawili cha muda mrefu," alisema. Rukia Shaban aliishukuru DAWASA kwa kusikia kilio chao na kuleta mradi ambao utawapatia unafuu katika maisha.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kumuua bibiye

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imemhukumu Emmanuel Kulwa (36) kunyongwa mpaka kufa kwa kosa la kuwaua babu yake Donadi Kasika (70) na bibi yake Kalekwa Kazembe (60) kwa kuwacharanga kwa mapanga na mashoka kichwani na kufariki dunia papo hapo kisha akawatumbukiza kwenye shimo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ntemi Kilekamajenga, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo la mauaji ya kukusudia pasipokuacha shaka yoyote.

Jaji Kilekamajenga alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo, ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili kama yake.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na mawakili wawili wa serikali Monika Matwe na George Masalo ambao walipeleka hapo mahakamani mashahidi watano na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo aliwaua babu yake Donadi Kasika (70) na bibi yake Kalekwa Kazembe (60) kwa kukusudia.

Jaji Mfawidhi Kilekamajenga alisema upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea Raulent Mgoti ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa huyo ambaye alijitetea peke yake hakuwa na shahidi wala kielelezo.

Aidha Jaji Mfawidhi Kilekamajenga alisema shahidi wa Upande wa Jamhuri ambaye ni Mtoto wa Marehemu hao Elizabert Mashauri (45) alisema Machi 29 mwaka 2020 majira ya saa 8 mchana akiwa nyumbani kwake, watu watatu walifika na kumwambia kwamba pale katika Shule ya Msingi Bukori tumeona nguo za mama yako Kalekwa Kazembe zikiwa na damu, nguo hizo ni shuka, gauni na kanga.

Alisema hapo mahakamani kuwa baada ya kupata taarifa hizo aliongozana na watu hao hadi sehemu ya zilipokuwepo nguo za mama yake mzazi, baada ya kufika alikuta watu wengi wamekusanyika hapo akiwemo na mshtakiwa Emmanueli Kulwa ambaye alikuwa akiishi na wazazi wake.

Aidha, Jaji huyo alisema alimuuliza mtoto wa dada yake Emmanueli Kulwa ambaye ni mshtakiwa kwamba nguo za mama yangu zimefikaje huku shuleni na wakati wewe ndiye unaishi na wazazi wangu, mshtakiwa alimjibu kwamba sijui. Baada ya kujibiwa hivyo alimuomba ufunguo wa nyumba ya wazazi wake, mshtakiwa huyo alitoa funguo mfukoni mwake na kumkabidhi shahidi huyo ambaye ni mama yake mdogo.

Aidha, alisema alipofika nyumbani kwa wazazi wake alifungua mlango wa sebuleni akakuta Panga, mkuki na shoka zikiwa na damu pamoja na chini karibu na mlango kuna damu na alifuatilia damu hizo hadi kwenye shimo na kukuta mama yake mzazi Kalekwa Kazembe (60) na baba yake Donadi Kasika (70) wametupwa humo na wameishafariki dunia na harufu mbaya inatoka.

Alisema baada ya kuona miili ya wazazi wake alianguka chini na kuzimia na alipozinduka aliambiwa na wanazengo kwamba njoo uone mama yako kwa mara ya mwisho, alipoamka alimuona mtoto wa dada yake Emmanuel Kulwa, amekamatwa na polisi na yuko kwenye gari la polisi, kutokana na miili hiyo kuharibika walizika usiku.

Aidha, alisema kesho yake ya Machi 30 mwaka 2020 alipata taarifa kwamba mtoto wa dada yake Emmanueli Kulwa ambaye ni mshtakiwa aliamua kuwaua bibi yake na babu yake ili achukuwe mashamba na ayauze ili akanunue pikipiki.

Alisema baada ya mshtakiwa huyo kukamatwa alipelekwa katika kituo cha polisi Bukori na alipohojiwa alikiri kuwaua bibi yake na babu yake, ili aweze kuuza mashamba ili anunue pikipiki.

Alisema uchunguzi wa Daktari unaonyesha kuwa marehemu wote walikuwa na majeraha ambayo yalisababisha damu nyingi kumwagika na kusababisha vifo hivyo na miili hiyo ya marehemu Donadi Kasika (70) na Kalekwa Kazembe (60), miili hiyo ilikuwa imeishaharibika kwa sababu ilikuwa imekaa muda wa siku nne ikiwa kwenye shimo.

"Kama mshtakiwa hakutenda kosa hili aliwezaje kupata ufunguo wa nyumba ya marehemu hao, mimi nimeridhika kweli kwamba mshtakiwa alitenda kosa hili pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa la mauaji ya watu wawili."

"Baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani, Mahakama, hii inakuhukumu mshtakiwa Emmanueli Kulwa kunyongwa mpaka kufa na Rufaa ipo wazi, lakini mimi nimekuona umetenda." alisema Jaji Kilekamajenga.

Awali, akisoma hati ya mashtaka jana Msaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Jackline Samweli alidai kuwa Machi 29 mwaka 2020 katika kijiji cha Bukori kitongoji cha Chirungure mkoa wa Geita mshtakiwa aliwaua babu yake Donadi Kasika (70) na bibi yake Kalekwa Kazembe (60) kwa kuwacharanga kwa mapanga na mashoka kichwani na kufariki dunia papo hapo kisha akawatumbukiza kwenye shimo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.





# Mbunge awaonya wahitimu ufadhili wa masomo ughaibuni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MBUNGE wa Singida Mjini, Mussa Sima, amewatahadharisha wahitimu wa kidato cha sita kujiepusha na ufadhili wa masomo nje ya nchi unaolenga kushawishiwa wajiingize kwenye mahusiano ya mapenzi ya jinsia moja.

Sima alitoa hadhari hiyo juzi kwenye mahafali ya 48 ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida.

Alisema sasa hivi zinatumika mbinu mbalimbali na mataifa ya magharibi kuwashawishi wananchi kujiingiza kwenye masuala ya ushoga, hivyo hata suala la ufadhili wa masomo linaweza kutumika kama njia mojawapo ya kuwashawishi watu.

Mbunge huyo alisema serikali haikubaliani na mambo hayo lakini mitandao ya kijamii imetoa nafasi ya mtu kufanya chochote, lakini kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imezuia vitu ambavyo havina maadili na utamaduni wa kitanzania.

"Kutokana na kukua kwa teknolojia mtu anaweza akaingia kwenye mitandao ya kijamii na kukutana na vitu hivyo vikiwepo kupata fedha au ufadhili wa masomo na bila kujua anajiingiza kujaza fomu kupatiwa ufadhili wa masomo au kazi na kutumiwa fedha na tiketi ya ndege,"alisema.

Mbunge Sima alisema watu hao wakija na mbinu hizo za kutoa ufadhili wa masomo katika vyuo mbalimbali nje ya nchi walengwa wanatakiwa kutoa taarifa kwa wizara husika ambayo inavijua vyuo vyote hivyo ili kupata uthibitisho badala ya kwenda kimya na kujikuta wakiharibikiwa.

Aidha, Sima aliwataka wazazi na walezi wa wahitimu hao watakapokuwa nyumbani wakisubiri matokeo yao kuwapa stadi za maisha kwa kuwafundisha shughuli mbalimbali za nyumbani ikiwemo ujasiriamali na kilimo.

Mkuu wa shule hiyo, Method Njiku alisema wameendelea kufanya vizuri na kushika nafasi ya juu katika matokeo ya mitihani ya taifa na mikakati waliyonayo ni kuondoa daraja la nne na kubakiwa na daraja la kwanza na la pili.



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk. Khamisi Mkanachi akisalimiana na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Bicha, katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa, mkoani Dodoma alipotembelea juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TMDA yateketeza dawa, vifaa tiba visivyofaa matumizi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Kati imeteketeza shehena ya dawa na vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi ya binadamu na mifugo vyenye thamani ya Sh. milioni 28.5.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Ofisa kutoka TMDA Kanda ya Kati, Emmanuel Ndejembi alisema dawa hizo zinajumuisha zilizoisha muda wa matumizi na zisizo na usajili nchini ambazo zilikamatwa na kuondolewa katika soko.

Ndejembi alisema kuwa shehena hiyo ilipatikana kupitia ukaguzi uliofanywa na mamlaka kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2022.

Alisema kuwa dawa hizo zimekamatwa katika halmashauri mbalimbali zilizopo ndani ya mikoa ya Singida,Iringa,Dodoma na Morogoro.

Ofisa huyo alisema kuwa wamiliki wa maeneo ya kutolea huduma za dawa na vifaa tiba walibainika kukiuka matakwa ya sheria na wamewajibishwa kwenye ukaguzi huo kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa na serikali ili kuuza bidhaa hizo zikiwa na ubora, usalama na ufanisi kwa lengo la kuendelea kulinda afya za wananchi.

Pia, aliwaasa wananchi kuhakikisha wanakagua dawa kabla ya matumizi ili kuepukana na kuuziwa au kutumia dawa na vifaa tiba visivyokidhi vigezo vya ubora na usalama kwa binadamu na mifugo.

# Kamati ya Bunge yaagiza bajeti ya usalama, afya kuongezwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeishauri serikali kuongeza bajeti ya usimamizi wa masuala ya usalama na afya ili kuuwezesha Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), kuzuia ajali, magonjwa na uharibifu wa mali katika shughuli za uzalishaji hususani miradi mikubwa ya maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa jana bungeni baada ya OSHA kuwasilisha randama ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na taarifa ya muundo na majukumu yake mbele ya kamati hiyo inayoisimamia Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi chini yake wakala huo.

Akizungumza baada ya kuhitimisha kikao hicho, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Riziki Lulida, alisema OSHA ina jukumu kubwa la kusimamia mifumo ya kuzuia ajali na magonjwa katika maeneo ya kazi, hivyo kupelekea shughuli za uchumi kufanyika kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Alisema ili kufanikisha jukumu hilo serikali haina budi kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha kufanya kazi yake ipasavyo hususan katika miradi mikubwa ya mafuta na gesi ambayo inahitaji kushughulikiwa kwa umakini mkubwa ili kuepuka madhara makubwa yatakayotokea endapo ajali zitatokea katika maeneo husika.

"Uwepo wa OSHA ni mkakati wa maendeleo ya wafanyakazi na usalama wa nchi lakini watu wengi wanakwepa kutekeleza taratibu za usalama na afya kwenye maeneo ya kazi.

Hivyo, sisi tunaishauri serikali isimame imara na iwape OSHA bajeti ya kutosha ili kufanya kazi ya kuisaidia nchi,"alisema.

Aidha, Kamati hiyo ilibainisha kwamba OSHA imeleta mabadiliko makubwa katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ikiwemo sekta ya mafuta na gesi.

"Mafanikio ya OSHA ni makubwa sana endapo tukiangalia tulikotoka ambapo wafanyakazi walikuwa hawajui haki zao za msingi kuhusiana na masuala ya usalama na afya mahali pa kazi."

"Katika vituo vingi vya mafuta tulikuwa tunaona vijana wakitoa huduma bila kuzingatia matumizi sahihi ya vifaa kinga kama vile viatu maalumu vya usalama (safety boots) badala yake walikuwa wanavaa ndala au lakini sasa hali imebadilika na vituo vingi wanazingatia taratibu muhimu za usalama na afya," alisema Mariamu Kisangi, Mjumbe wa Kamati.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema amefarijika kuona wawakilishi hao wa wananchi wanatambua kazi kubwa inayofanywa na OSHA katika kusimamia uzingatiaji wa taratibu za usalama na afya kwenye maeneo ya kazi nchini.



## SMZ yaingia makubaliano usimamizi Kisiwa cha Mnembe

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetiliana saini mkataba wa usimamizi wa eneo la Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba na Kampuni ya Beyond ambao utasaidia kuongeza makusanyo.

Akizungumza jana baada ya utiaji wa saini wa makubaliano hayo Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame, alisema makubaliano hayo yataongeza idadi ya makusanyo ya idara ya uhifadhi wa bahari kutoka Sh.bilioni 1.2 hadi Sh.bilioni tatu kwa mwaka 2023/2024.

Alisema kwamba mapato hayo yataongezeka kama serikali itaridhia upitiaji upya wa tozo kutokana na shughuli mbalimbali na michezo ya watalii yanayofanyika baharini.

Aidha, alisema tozo ambazo zinatolewa kwa sasa ni ndogo ikilinganishwa na tozo za nchi nyingine kwenye ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi.

"Ongezeko hili la mapato litakalotokana na mkataba huu lina faida kubwa kwa jamii iliyo ndani ya Hifadhi ya Mnemba (MIMCA), kwa sababu asilimia 30 ya mapato yatakayokusanywa inarudi kwao kutatua changamoto zao mbali mbali za kimaendeleo na za uhifadhi wa rasilimali Bahari," alisema Makame.

Hata hivyo alisema mapato hayo yataongezeka iwapo watapata ushirikiano wa wananchi wanaofanya shughuli zao ndani ya bahari. Aidha, alisema itaandaa utaratibu maalumu kuhakikisha mapato ya nchi hayapotei kiholela na kila kampuni kuona inalipa kwa mujibu wa sheria.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Aboud Sulaiman Jumbe alisema hifadhi ya bahari ni muhimu kwa mazingira ya nchi na ndiyo chachu ya falsafa ya uchumi wa buluu na maendeleo yake.

Alisema mkataba huo utaongeza mnyororo wa thamani pamoja na pato la taifa na itakuwa na chanzo chake kipya cha mapato.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya Beyond, Jane Brack, alisema kuwa ushirikishwaji huo unaenda kutoa tija za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya bahari ya Kisiwa cha Mnemba.

# SMZ yawaita wawezekezaji kwenye uchumi wa buluu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema imefungua milango ya kuwakaribisha wawekezaji kunufaika na fursa zinazopatikana kutoka sekta mbalimbali za maendeleo ikiwemo uchumi wa buluu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na wawekezaji kutoka Uingereza wakiongozwa na Agnes Gitau wa Taasisi ya Eastern Africa Association.

Dk. Mwinyi aliueleza ugeni huo kwamba Zanzibar imejikita zaidi kwenye ajenda yake ya uchumi wa buluu ambako kuna fursa nyingi kwa wawekezaji ikiwamo uvuvi na kilimo cha mwani baharini. Aliwashauri wawekezaji hao kuangalia uwezekano wa kuweka nguvu eneo hilo ili kutoa mchango utakaowainua wavuvi nchini.

Rais Dk. Mwinyi, alisema Zanzibar mbali ya kubarikiwa na bahari yenye ufukwe na zenye kuwavutia wageni pia ina ushindani wa biashara na uwekezaji kwa sekta mbalimbali za uchumi na utalii.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliwashauri wawekezaji hao kuzungumza na Mamkala ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) wenye jukumu la kushughulikia masuala yote za uwekezaji nchini.

Dk. Mwinyi aliueleza ugeni huo kwamba kwa sasa taasisi hiyo inafanya kazi kwenye mwamvuli mmoja na tasisi zote zinazotegemeana, kukamilisha taratibu zote za uwekezaji nchini ili kurahisisha mchakato wa taratibu hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Eastern Afrika Association, Agnes Gitau alisema lengo la ujio ni kuangalia na kuzitumia fursa zilizomo kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa biashara pamoja na kuzungumza na baadhi ya wawekezaji kutoka sekta binafsi.

Meneja wa Mfuko wa Rasilimali Endelevu (ARCH) kutoka Uingereza, Amanda Van Dyke, alisema matarajio yake kushirikiana na asasi mbalimbali za kiraia zilizopo Zanzibar na kuahidi watashirikiana kwenye maeneo mbalimbali.




Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulghulam Hussein (wa pili kulia), akikabidhi zawadi kwa Mwanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Mariam Rajab Othman baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa shindano la insha kuhusu umuhimu wa viwango, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika, jijini Zanzibar juzi. Wa tatu kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), Yusuf Nassor. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ: Tunatambua mchango wa wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulghulam Hussein, amesema kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), inatambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza viwango nchini na Afrika kwa ujumla.

Alieleza hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika yaliyofanyika Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa kuwawezesha wajasiriamali wadogo kwa kuwapatia fedha za kuendesha biashara zao ili kujipatia kipato cha kujikimu na kukuza mitaji yao na kuzalisha ajira.

Aidha, alisema vyuo vikuu vinamchango mkubwa katika kukuza tasnia hiyo kwa kufanya tafiti, kuzalisha wataalamu na wabunifu watakaochochea maendeleo.

Hivyo, aliwataka wakuu wa vyuo vikuu vya Zanzibar kuendelea kuhamasisha wanafunzi juu ya suala la ujasiriamali akisema jambo hilo litawasaidia vijana kujiajiri na kukuza kipato chao.

Aidha, aliitaka ZBS kubeba jukumu la kuandaa viwango vinavyohitajika na kusimamia utekezaji wake ili kukuza soko la bidhaa za wajasiriamali na kuona bidhaa hizo zinakuwa na ubora unaohitajika.

Alisema serikali inaendelea kuchukua juhudi za kuhakikisha kuwa bidhaa za wajasiriamali zinakuzwa na kupatiwa soko la uhakika, huku changamoto wanazokabiliana nazo zinazingatiwa na kutatuliwa.

Akizungumzia mashindano ya insha yanayoandaliwa na Shirika la Viwango Afrika (ARSO) kupitia taasisi za viwango za nchi wanachama, aliipongeza ZBS kwa kutekeleza jukumu hilo kwa Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Rashid Ali Salum, alisema serikali inahitaji wataalamu kwa ajili ya kufanya kazi katika tasisi hiyo, hivyo suala la elimu lina umuhimu mkubwa.

Hivyo, aliitaka ZBS kuhakikisha inachukua jukumu la kutoa elimu zaidi kwa wananchi na wafanyabiashara kuliko adhabu ili kuwawezesha wafanyabiashara kujua umuhimu wa viwango.

Mkuu wa ZBS, Yussuph Majid Nassor, alisema wanachama wa ARSO ikiwemo taasisi hiyo kila mwaka husherehehekea kwa kuitisha shindano la uandishi wa insha.

Alisema wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Zanzibar huandaa isha kwa kutumia kauli mbiu ya maadhimisho ambapo mchakato huo ulianza Januari na jumla ya insha 44 zilizoandaliwa na vyuo 13 vya Zanzibar ziliwasilishwa na kupatikana washindi 10.







Nipashe
BT
BURUDANI TELE



# KACHAMBA KIUME

MWANAMUZIKI maarufu nchini, Barnaba, ameingia katika orodha ya waimbaji waliotumia nyimbo kuwasema wale wanaoonekana kuingilia maisha yao.

Hivi karibuni Barnaba, alionekana kusakamwa kwa maneno tofauti kuhusu hatua yake ya kubadili dini kuwa muislam.

Kulikuwa na maoni tofauti baada ya kuchukua uamuzi huo, kuna wale waliomtakia heri katika imani yake mpya, na kuna baadhi walimsakama kwa kudai kuwa mchumba wake Raya ndiye aliyemshawishi.

Kupitia kibao chake kipya 'Nampenda' mwimbaji huyo amesema mjadala huo kwake hauna maana kwani uamuzi wake huo ni jambo la kawaida katika jamii.

Ndani ya wimbo huo msanii huyo amesema kwamba yeye na Raya wanapendana, licha ya kuachana na kurudiana mara kadhaa, penzi lao limerudi upya na hakuna wa kumwacha mwenzake.

Barnaba amesema watu hawajui alipotoka na Raya kwani kuna baadhi ya watu wanajifanya wanawajua sana kama wao ndio wazazi wao.

"Mopawa kawa Mohamedi kisa mapenzi,Kipi cha kuwashangaza maisha yetu yanawahusu nini?

Kama Mungu tunayemuwabudu sote ni mmoja

iwe pepo iwe moto sote njia yetu moja."
Imesema sehemu ya wimbo huo.

BASI SAWA

## Gigy Money ajutia mdomo



MWIMBAJI wa Bongo Fleva, Gigy Money, amesema ulikuwa utoto kuropoka maneno ambayo yaliwaudhi baadhi ya wasanii akiwemo Ali Kiba.

Akizungumza hivi karibuni, amesema tatizo lake lilikuwa kuzungumza ukweli katika muda usio sahihi, kiasi ambacho wengi walimchukia na kumuona kama mchafuzi wa mambo.

"AliKiba nilimuomba msamaha nafiri amenisamehe kwani siku hizi tukionana anatabasamu tofauti na zamani, namkumbuka sana kwani ana roho nzuri, sio mchoyo yeye ndiye aliniita Nick Minaj," amesema Gigy.

## Suma Mnazareti kasema neno



RAPA mkongwe Suma Mnazareti, amesema muziki wa Bongo Fleva hauna mdundo wake maalum, kinachofanyika sasa ni kupiga mahadhi ya nchi nyingine.

Suma amesema wasanii hawawezi kujitenga na muziki wa nje kutokana na kuwa hakuna muziki wa asili ya Tanzania wanaoweza kujivunia na kusema ni wao pekee kama ilivyo nchi nyingine za Afrika.

"Hatuwezi kujiepusha na muziki wa nje kama Afrika Kusini na Nigeria, sisi hatuna midundo inayotutambulisha na ni lazima kuendelea na hali hii mpaka tupate aina yetu ya muziki tunaoweza kusema huu ni wa kwetu," amesema.



## Kayumba hana kinyongo

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Kayumba amesema hajaumizwa kutokana na baadhi ya mastaa kutohudhuria katika uzinduzi wa albam yake hivi karibuni.

Akizungumzia suala hilo, amesema kila kitu kilienda vizuri na kuna baadhi walimuomba radhi kwa kutofika na wengine walichelewa kutokana na sababu mbalimbali.

"Namshukuru Mungu kila kitu kilikwenda vizuri, kutokuja kwa Harmonize na Ali Kiba si suala la kuniumiza moyo kwani wote walikuwa na sababu tofauti ambazo wasingeweza kufika pale, kizuri tupo pamoja," amesema Kayumba.

# Limbwata: Mapenzi yenye usaliti

**Na Adam Fungamwango**

INAAMINIKA kuwa limbwata ni dawa ya kiasili ambayo wanatumia kinadada au kinamama 'kuwatengeneza' wapenzi au waume zao wawe wanawatii na kuwasikiliza.

Pia inasemekana huwatuliza wanaume macho juu, vicheche na wanaohangaika na dunia ambao ni kama vile samaki hapishi chambo.

Hata hivyo, inasemekana wakati mwingine dawa hiyo huenda mbali zaidi na kumfanya mwanaume kama mtu aliyechanganyikiwa au zezeta kitu ambacho kinageuka kuwa kero kwa mwanamke aliyefanya hivyo.

Dhana hii ipo miongoni mwa jamii na hata kumekuwa na simulizi nyingi zikihusiana na kitu kama hicho, na zipo riwaya, tamthilia na filamu ambazo zinalizungumzia jambo hilo ambalo bado halina uhalisia wa moja kwa moja.

Leo tunaiangalia filamu iitwayo 'Limbwata'. Imechezwa na wasanii mbalimbali ambao majina yao ya kisanii waliocheza kwenye picha hilo ni Margareth Komba (Amanda), Omari Yadilu (Kibanzi), Irene Midelo (Midelo), Sakina Charambo (Bosi), Malya Lawrence (Malya), Carlos Luvanda (Kijana), Delila (Ovina), Joha Msham (Didi), Chuma Muddy (Chuna), Salim Zuberi (Sam), Omari Mtomea (Mtomea) na Sharifa Mimbi (Fefe).

Amanda, mke wa Kibanzi anapigana na dada mmoja jirani akimtuhumu kuwa anamchukulia mumewe. Hata hivyo zilikuwa ni hisia tu.

Shoga yake akamtuhumu kukaa kizembezembe, akitaka amfanyie dawa ili atulie amfanyie kitu kinaitwa limbwata.

Akamwambia kama anataka mwamume awe wake peke yake ni ngumu sana, ila kuna njia ya kufanya na kumfanya ampe chochote anachokitaka hata kama hana. Kitu hicho kinaitwa limbwata, dawa ya kuwafanya wanaume wakorofi, vicheche na macho juu juu kutulia kama maji ya mtungini kwa yule ambaye amemfanyia hivyo.

Amanda anaufanyia kazi ushauri wa shoga yake, akafanya dawa ya kumpumbaza mumewe Kibanzi ili ampende yeye peke yake, asihangaike kwa wengine. Anafanikiwa. Mume sasa kazini kukawa hakuendeki. Kila siku anakuwa na dharura, anaaga kwenda nyumbani. Na huko hakuna chochote, anachotaka ni kukaa tu na mkewe. Kazini nako hali ikawa tete. Mtoro, akaachishwa kazi. Hakuna mbaya kwake, yeye alichotaka akae nyumbani kwa mkewe. Mke sasa kaanza kuona kero.

Mke sasa akaamua kufanya biashara ili amlishe mume. Mume akaamua kufanya biashara ya kuuza maji kwenye madumu wakati awali alikuwa anafanya kazi ofisini. Ikabidi mke aamue kumueleza ukweli mumewe kisa kilichofanya awe kwenye hali hiyo, wivu ulifanya kumuwekea limbwata, yakaharibu maisha ya wote wawili, hivyo akajutia kitendo hicho na kuomba radhi.







## Lukamba kumbe mwigizaji

ALIYEKUWA mpiga picha wa Diamond, Lukamba amesema kuonekana katika sanaa ya uigizaji sio jambo geni, kwani kabla ya kuingia fani yake ya picha alikuwa akiigiza filamu.

Lukamba amesema kujikita katika filamu sio kwamba ameshindwa kazi yake ya upigaji picha katika muziki, bali ni kutekeleza ndoto zake za kila siku kuwa msanii mkubwa katika tasnia hiyo.

Katika siku chache zijazo Lukamba anatarajiwa kuonekana katika tamthilia mpya ya Jeraha inayowahusisha wakongwe kama Chuchu Hans na Ray Kigosi itakayorushwa katika chaneli ya sinema zetu.

## LOKASA YA MBONGO KILIO KWA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

HAIKUWA wiki nzuri kwa mashabiki na wapenzi wa muziki wa dansi Afrika na dunia nzima, zilipotolewa taarifa za kifo cha mwanamuziki maarufu kabisa Denis Lokassa ambaye umaarufu wake anajulikana kama Lokassa ya Mbongo.

Mwanamuziki huyo mkongwe na maarufu barani Afrika na dunia kwa ujumla, akiwa mpiga gitaa la 'rhythm', alifariki dunia usiku wa Jumanne kuamkia Jumatano nchini Marekani akiwa na miaka 80, baada ya kuugua kwa muda mrefu, akisumbuliwa na ugonjwa wa kisukari na kupooza.

Mwanamuziki mwenzake Mekanisi Modero amesema amepokea taarifa za msiba wa Lokassa kutoka kwa mhudumu wa afya ambaye alikuwa akimuuguza.

"Alikuwa akipumua kwa shida kabla ya mauti kumfika katika mji wa Nashua New Hamshire nchini Marekani," alisema.

Kwa Watanzania, anakumbukwa kuwa aliwahi kuja mara kadhaa miaka ya 1990 akiwa na bendi yake ya Soukous Stars, akiwa kiongozi wa kundi hilo.

Ni miaka ambayo yeye na kundi lake hilo lililokuwa na kina Dally Kimoko, Ngouma Lokito, Yondo Sister, Ballou Kanta, Lucian Bokilo, Shimita Lokombo Nzambi, Saladin Ferreira na wengineo walitamba sana na aina yake ya muziki iliyowachanganya sana mashabiki wa muziki si Tanzania tu, bali Ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati.

Mwanamuziki huyo alianza kutengeneza jina akiwa na Tabu Ley Rochereau kwenye bendi Afrisa International kuanzia mwaka 1970 hadi 1978.

Mashabiki wa muziki wa dansi nchini wameonyesha kusikitishwa mno, kwani nyimbo zake zilitamba mno kwenye miaka ya 1990.

Hizi ni baadhi ya nyimbo zilizopagawisha Wabongo.

**KAFUL MAYAY**

Huu ndiyo wimbo ambao watoto wa mjini wanasema ulimtoa. Ulitamba sana Bongo. Pamoja na ufundi wa mwanamuziki Tabu Ley kuuimba kwa sauti yake tamu, lakini gitaa la 'rhythm' lilitawala na kuupamba zaidi wimbo huo uliofyatuliwa mwaka 1973 na kuufanya kuwa wa kuvutia. Lokasa ya Mbongo ndiyo alipiga gitaa hilo na baada ya hapo ni kama vile alianza kupata fursa.

**MONICA**

Huu ni wimbo uliokuwa maarufu sana, ulikuwa ukipigwa kila kona ya hapa Tanzania na kwenye sherehe za kijamii hukosi kusikia 'Monica eee eee, Monica ooo.' Aliutoa mwaka 1985 akiwa na bendi yake ya Soukous Stars kama kawaida yeye yupo kwenye gitaa ya kati 'rhythm'.


**MARIE JOSE**

Ni moja kati ya nyimbo zake zilizotamba sana kwenye sherehe mbalimbali za kijamii nchini, uliotoka mwaka 1986 kiwa na bendi yake ya Soukous Stars.

**SOPHIA**

Shughuli pevu aliifanya kwenye albamu ya 'Morenita' ambapo yeye na wenzake kina Yondo Sister mwaka 1990 walitoa ngoma zote kali ndani ya albamu hiyo ambazo zilitetemesha Afrika. Kwenye albamu hiyo hayati Lokassa ya Mbongo akitunga wimbo uitwao 'Sophia.' '...Sophia, i love you mwana mama..." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo ulioimbwa kwa ustadi na Shimita.

**NAIROBI NIGHT**



Huu ndiyo wimbo maarufu na uliopendwa zaidi Bongo. Usipoupiga kwenye shughuli yoyote basi haijaisha hiyo. Wimbo huo mrefu, wa dakika 15 na sekunde 44, umekusanya nyimbo nyingi za bendi mbalimbali za Tanzania na Kenya.

Lokasa ya Mbongo, akiliongoza kundi lake la Soukous Stars alizikusanya nyimbo kama 'Dada Asha' wa Tabora Jazz, 'Vigelegele' na 'Roza' wa Western Jazz zilizorekodiwa miaka ya 1970. Utofauti ni kwamba mkusanyiko wa nyimbo hizi na ulitangeneza wimbo mmoja ulioitwa 'Nairobi Night', uliofyatuliwa mwaka 1994, ulikuwa na mapigo ya kasi na kurekodiwa kisasa zaidi.



# Phyna utabe baje dola nje nje?

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Phyna, ameutaka uongozi wa hoteli ya Asaba, kurudisha pesa zake baada ya kuibiwa wakati akirekodi filamu.

Nyota huyo amesema kuwa alikwenda hapo baada ya kuunganishwa na mwigizaji na mtayarishaji wa filamu, Destiny Etiko, siku chache zilizopita.

Amsema alikutana na Etiko ili kurekodi filamu, inayoitwa 'Unholy Stain.'

Amedai kuwa dola zake ziliibiwa ndani ya begi lake na muhudumu wa hoteli ya Asaba, aliyokuwa akiishi.



## Skales ampigia goti mkewe

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Skales amemuomba msamaha mke wake baada ya kumwita jina la shetani miezi michache iliyopita.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Skales alimuomba radhi mke wake Precious wakati akifurahia siku yake ya kuzaliwa, akieleza kauli hiyo ilimtoka kwa bahati mbaya.

Skales pia alimkosoa mke wake kwa kuwatapeli watu kuwa alifiwa na mama yake wakati ndoa yao ikiwa na muda wa mwaka mmoja.

## Joeboy bora ungeoa kabisa

NYOTA wa muziki wa Nigeria. Joeboy amefichua kuwa ametumia zaidi ya Naira milioni 50 kwa mpenzi wake katika miaka miwili iliyopita.

Alipokuwa akijibu maswali kuhusu umri wake mdogo na kujihusisha kwenye mapenzi, Joeboy alithibitisha kwamba anapenda kumtendea mwanamke wake kwa wakati mzuri na hasiti kumgeuka.

"Umesema kweli. Ninapenda kumuhudumia mwanamke wangu, pesa ambazo nimemtumia, tuseme zaidi ya Naira milioni 50," amesema Joeboy.





## Gavor hongera sana

MWIGIZAJI na mtangazaji wa Tv kutoka Ghana, Mawuli Gavor na mpenzi wake mwenye asili ya India, Remya Gavor, wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Habari hizo njema zimetolewa na msanii huyo kwa ajili ya mashabiki zake kupitia ukurasa wake wa Instagram, wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Katika salamu zake kwa mashabiki zake ameandika " Ni mwaka wa kuwa mzee, wakati bado kijana,".

## Tekashi aponzwa na mdomo

KIPIGO alichokipata rapa Tekashi, kimeelezwa hakikuwa cha kitoto kwani msanii huyo inaelezwa amevunjika mgongo na mbavu.

Taarifa zinasema kuwa Tekashi amelazwa Hospitali baada ya kuvamiwa na kundi la watu na kisha kupigwa wakati akiwa eneo la mazoezi huko Florida.

Wakili wa rapa huyo, Lance Lazzaro, ameiambia TMZ kuwa jamaa amejeruhiwa sana na kwamba madaktari wanaendelea kumpa matibabu.

Mashabiki wake wengi wanaamini kundi la washikaji zake wa "Nine Trey Gangsta Bloods" waliosababisha waende jela mwaka 2020 na yeye kuachiwa huru wanahusika na tukio hilo.





## Mradi ujenzi wa mazizi bora kunufaisha kaya 1,700

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MRADI wa ujenzi wa mazizi bora ya mifugo unaotekelezwa na Shirika la TPW, utazinufaisha kaya 1,700 zilizoko katika wilaya nne za Mkoa wa Manyara, ili kuinusuru mifugo yao kuliwa na wanyama.

Shirika hilo la TPW linalenga kumaliza tatizo la mifugo ya jamii za kifugaji kuliwa na wanyama wakali, huku pia likilinusuru eneo la nyanda za malisho, lenye ukubwa wa hekta 1,600 kwa kung'oa mimea vamizi.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Babati na wadau wa uhifadhi, wafugaji, viongozi wa kimila na viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji hadi wizara, Mkurugenzi wa TPW, Neovitus Sianga, alizitaja wilaya zinazonufaika na mradi huo ni Babati, Longido, Simanjiro na Monduli.

"Tunawajengea wafugaji mazizi imara ili kudhibiti wanyamapori kuvamia mifugo,"alisema Sianga

Aidha, alisema shughuli mojawapo ambayo wamekuwa wakishiriki ni kupunguza migogoro ambayo inawakumba watu na wanyamapori ambao huathiriwa na wanyama wanaokula nyama.

Kuhusu mmea vamizi unaosumbua wafugaji alisema unaitwa mtundulu na athari zake unachukua maeneo makubwa ambayo yanatumiwa na wafugaji na wanyamapori.

Mshauri wa TPW, Alais Morindat, alisema ikiwa malisho yameliwa na yako chini itaacha ardhi ikiwa wazi na mimea mingine vamizi itaota kwa haraka.

Kwa mujibu wa Morindat, mimea hiyo vamizi inayong'olewa katika wilaya hizo ni ile ambayo hailiwi na wanyama.

Kiongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya kimasai, Laigwanani, Komite Iyasi (Monduli), alisema TPW inawasaidia kupata malisho, kwamba katika eneo lake wamewawezesha kung'oa mimea vamizi eka 70 na yeye amejengewa ukuta hai kwenye zizi lake, hivyo fisi na wanyama wengine hawawezi kuingia. Kwa upande wake, Ofisa Usimamizi Nyanda za Malisho kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Alfred Mushi, alisema ili kukabiliana na nyanda za malisho yamejengwa mabwawa 10 na kuanzishwa mashamba darasa 100 nchi nzima kwa mwaka uliopita.

# Mahakama yawaita wajibu maombi kesi kutoweka mkazi

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, imetoa hati ya wito ya kuitwa shaurini kwa wajibu maombi katika kesi ya kupotea kwa Mkazi wa Kijiji cha Ololosokwani, Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro, Oriais Oleng'iyo (85).

Wajibu maombi katika kesi hiyo ni Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha (RPC), Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Ngorongoro (OCD).

Hati hiyo ya wito wa kuitwa shaurini ilitolewa jana na Jaji Mohamed Gwae anayesikiliza shauri hilo.

Juzi, kesi hiyo ilishindwa kuendelea mahakamani humo kutokana na mawakili wa wajibu maombi (mawakili wa Jamhuri) kutoonekana mahakamani hapo. Jaji Gwae alitoa siku chache kwa wajibu maombi kufika mahakamani, huku akiagiza mawakili wa waleta maombi, Joseph Shangai, William Ernest na Simon Mbwambo, kufika mahakamani humo na mteja wao ambaye ni mtoto wa Oleng'iyo anayedaiwa kutoonekana. Tangu kukamatwa kwa wananchi 19 wa Loliondo na baadae kesi yao kufutwa, Oriais Oleng'iyo, peke yake hadi sasa inadaiwa hajulikani aliko.

Jaji Gwae aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 30 mwaka huu, itakapoanza kusikilizwa.

Waleta maombi katika kesi hiyo wanaiomba mahakama hiyo, iamuru wajibu maombi kumpeleka mahakamani, Oriaisi Ng'iyo, ambaye amepelekwa kusikojulikana tangu alipokamatwa nyumbani kwake, Engong'u Nairowa, Kata ya Ololosokwan, Loliondo Wilaya ya Ngorongoro.

Pia, wanaiomba mahakama iamuru au kuwaelekeza wajibu maombi kumwachia huru, Oriasi Kurosawa, ambaye anashikiliwa tangu Juni 10, mwaka jana.

Vilevile wanaiomba mahakama hiyo iamuru walalamikiwa waende mahakamani kueleza sababu za kumshikilia Oriasi Ng'iyo, kinyume cha sheria.

Ombi lingine wanaiomba Mahakama iamuru na kuelekeza wajibu maombi kuupeleka mwili wa Oriaisi Ng'iyo, akiwa hai au asipokuwa hai.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Juma Irando (kushoto), akipata maelezo ya hali ya ugonjwa wa kifua kikuu kutoka kwa Mratibu wa Mwitikio wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukimwi Tanzania wa mkoa huo, Zakaria Mhina wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani humo jana. Wa (pili kushoto) ni Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Frola Kessy na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Desderia Haule. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mil.700/- zatengwa kumaliza kero ya maji vijiji vinne

**Na Anjela Mhando,** SIHA

SERIKALI imetenga Sh.milioni 700 kwa ajili ya kutatua kero ya upungufu wa maji kwa wakazi wa vijiji vya Ndinyika, Lekrumuni, Kandashi na Mawasiliano katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Mradi huo wa ujenzi wa miundombinu ya maji unatekelezwa na Kampuni ya Posh Alliance Limited na unatarajiwa kukamilika Aprili 15, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana na Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wilayani humo, Kondo Juma, kwa Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Christopher Timbuka, inaeleza kuwa mradi huo utawanufaisha wakazi hao ambao kwa idadi kubwa ni wa jamii za kifugaji. "Kimsingi kinachofanyika ni upanuzi wa skimu ya Gararagua kutoka Tantred Farm kwenda kwenye vijiji hivyo. Fedha za kutekeleza mradi huu ni mkopo kutokana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona na Mfuko wa Maji wa Taifa." alisema.

Mradi huo ulianza kutekelezwa rasmi Desemba 12 mwaka 2021, umefikia asilimia 98.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Magadini/Makiwaru, Monika Kimbi, aliagiza mradi huo kumalizika kwa wakati ili watu wapate maji kwa wingi na kujiletea maendeleo.

Grace Mollel na Neema Lukumay, ambao ni wakazi wa maeneo hayo kwa nyakati tofauti wakizungumzia mradi huo, walieleza namna ambavyo wamekuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilometa 15 kufuata maji vijiji jirani.

Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Christopher Timbuka, alisema: "Ili mradi huu uweze kuishi kwa muda mrefu mradi huu, msifanye hujuma wa kutoboa mabomba ili mpate maji ya wanyama. Huo ni ubinafsi, ilindeni ikiharibika maji mnakosa nyie sio sisi."

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

## WENYE ZAMA WAFUNGUKA...

# Klabu za mchangani zilivyokamata kila kona, wenye mitaa yao huwaambii kitu

## - Ndiyo mashabiki, wachezaji na 'watemi'

**Na Adam Fungamwango**

SIKU kama ya leo, lakini wiki iliyopita, tulikumbushana zama za soka la mchangani miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 lilivyonoga kushinda hata baadhi ya mechi za Ligi Kuu za sasa, hata vibanda umiza vinavyoonekana kushika umaarufu 'kiviiile.'

Toleo hilo halikuvuka kwa ukimya hivi hivi, wenye zama zao wakafumuka kutoka walikotoka, tabasamu mbele na maelezo kibao, mengine yalishakuwa sandukuni na yanaoza.

Ama kweli soka hilo halitofautiani na vyama vya siasa vya maeneo hayo, nguzo ya burudani na kwa watoto wa mjini hizo klabu zao zilikuwa ni kama sehemu ya imani yao, katika sura ile ile ya Simba na Yanga. Na kama huamini thubutu kuivuruga timu hiyo, iliyotimia kuanzia wachezaji, mashabiki, mabaunsa wake na hata 'maofisa utamaduni' nao walikuwa si haba. Kama ukweli ndiyo huo, wanapishana nini wanapishana nini na klabu hizo kubwa za soka nchini?

Kama ni mzaliwa wa tarehe za karibuni, nikuonjeshe kipengele kidogo tu, zilikuwepo klabu za soka za Ashanti na Boom FC za Ilala, Dar es Salaam, ambazo nilizigusia kidogo wiki iliyopita. Timu hizo pinzani zilibeba wasifu wote wa mechi za Simba na Yanga, lakini kwa kipengele cha Ilala, wakipata na wageni wasafiri wa mbali kutoka maeneo kama Magomeni, Kariakoo, Kinondoni, na Temeke, wakimiminika uwanjani kushuhudia mechi nzito.

Mechi zao zote zilikuwa zinachezwa kwenye Uwanja wa Karume, Dar es Salaam na dalili kuwa siku hiyo kuna mechi zilianza kuonekana mapema asubuhi tu pilika pilika zake na ikifika jioni inakuwa ni hatari.

Mara nyingi wakati inachezwa, nje na ndani ya uwanja waliokuwa wakilinda si askari wa kawaida, bali ni kikosi cha mbwa na farasi kutoka Ukonga ndicho kilichokuwa kikifanya kazi hiyo. Na wakati mwingine mechi hiyo inakuwa haimaliziki salama.

Ipo siku nitakuja kuelezea mtiti, vioja na songombingo ya mechi za Boom FC na Ashanti, ambapo kwa Dar walikuwa wanashika nafasi ya pili ukiondoa Simba na Yanga.

Nikudokeze tu, kila mahali kulikuwa na upinzani unaoendana na 'big match' kama hiyo ingawa wa Ilala ulizidi utamu wake, lakini kwenye mechi nyingi kubwa za mchangani wachezaji wote maarufu wanaochezea soka la juu, zikiwamo timu za Simba na Yanga, siku hiyo wanaonekana kurudi walikotokea, na hilo ndilo likajidhihirisha katika 'big match', kati ya Bongoyo na Eleven Stars katika Uwanja wa Magunia Msasani, winga hatari wa Majimaji na timu ya taifa, Celestine 'Sikinde' Mbunga, wakati akisikika anatua Jangwani kujiunga na Yanga, mwanzoni mwa miaka ya 1980, akaibukia kwenye mechi hiyo, akiichezea Eleven Stars, huku kama kawaida timu hizo zikitambishiana wachezaji wenye majina makubwa kama vile Yassin Maarufu wa Sigara na Athanas Michael wa Mlandege ya Zanzibar.



Tusiongee sana, tuwasikie wenyewe wenye zama zao wakifunguka:

Wa kwanza kabisa ni mwanahabari mkongwe Daniel Mkate ambaye alinipigia simu na kuniambia aliisoma makala ile, lakini akasema kuna baadhi ya timu maarufu ambazo hazikuwepo kama Friends Rangers ya Manzese, ambayo imetoa wachezaji wengi mno kwenye Ligi Kuu, mahasimu wao Kagera Rangers na Magomeni Kagera, DC Nyarugusu.

Ni kweli kabisa hizi ni moja kati timu maarufu sana zilizowatoa wachezaji wengi kama kina Mohamed Hussein 'Tshabalala', Shekhan Rashid, Thomas Kipese, Abdul Ramadhani 'Mashine', na wengine wengi.

Mkazi wa Magomeni aliniandikia meseji kwenye namba yake ya simu 0735 695662 akafunguka maneno haya.

"Mjukuu wangu Adam, katika timu za miaka hiyo, umezisahau New Boys na Jamaica za Magomeni Makuti, Sheffield Mzimuni, Wonder Boys ya Kanisani Magomeni Baptist (ilinzishwa na padri), Fighters Army ya Magomeni Mapipa, Bongoyo ya Msasani, Villa Equad, Jembe Sports ya Kinondoni Mkwajuni, Nungu Sports.

Msomaji mwingine anayeonekana ni mkazi ama wa Manzese au Tandale, yeye aliuliza kama timu maarufu wakati huo iliyowatoa wachezaji kama Hanzuruni Hamisi aliyekwenda kuichezea Simba na Sekelo Barnabas ambaye alizichezea klabu zote za Simba na Yanga, National kama ipo.

"Nilikuwa nauliza, hivi National ya Tandale bado ipo au imeshakufa?" Aliandika akitumia simu namba 0692 939282.

Mwingine anaonekana kipindi hicho alikuwa Tanga, akazitaja timu kadhaa za maeneo ya Majani Mapana.

Mchangiaji huyo mwenye namba 0765 477615 aliandika maneno haya:

"Mimi nazikumbuka klabu za Vipegi na Raidini zote za Majani Mapana, hawa ni mahasimu kweli kweli ambao walikuwa wakicheza kwenye Uwanja wa shule ya msingi Majani Mapana, timu zingine Tanga Mjini zilikuwa ni Vasco Da Gama, Rawalpind, Mzalendo, CIC, na Saruji."

Kuna huyu mwingine ambaye inaonekana alikuwa mkazi wa Msasani, naye akatoa maoni yake.

"Pia Msasani kulikuwa na klabu ya Elleven Stars ambayo ilikuwa ni mahasimu wakubwa na Bongoyo, ikiwa na wachezaji wenye majina makubwa kwenye timu kubwa, kuna Kumbukumbu ya Kinondoni."

Msomaji mwenye namba 0743 817900 alikumbusha timu za maeneo ya Tabata enzi hizo, akaandika.

"Kuna timu umesahau kama Joto ya Jiwe ya Tabata Kimanga, Twiga FC ya Tabata Kisiwani, National Housing ya Tabata Mawenzi, Tabata Boys ya Tabata Shule na pia Segerea United ya Segerea, ukiuliza watu wa miaka ya 1990 watawambia."

Hii yote ni kuonyesha makala ya toleo lililopita iliwakuna wengi na nikatoa nafasi kwa wasomaji kunikumbusha timu wanazozifahamu, lakini hazikuorodheshwa, hivyo wakaanza kupiga simu na kumimina meseji zao, wakikumbuka timu zao wanazozifahamu ambazo hazikuwepo.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Rwanda yadai kuna mauaji ya kimbari DRC

**KIGALI,** RWANDA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Vicent Biruta amesema nchi yake inahofu kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa mauaji ya kimbari dhidi ya raia wanaozungumza Kinyarwanda mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Akihutubia kikao cha kitaifa cha jukwaa la mashauriano cha kisiasa jana, Biruta aliilaumu jumuiya ya kimataifa kwa kushindwa kuchukua hatua kuzuia kuongezeka kwa ghasia.

Alisema ripoti kadhaa zimetolewa pamoja na ushahidi unaoonyesha ukweli wa uwezekano wa mauaji kama hayo kutokea.

"Kutambua mauaji ya kimbari kunakwenda sambamba na uwajibikaji wa kuyazuia yasitokee, baadhi ya wadai wa kimataifa wanasita kutambua mauaji ya kimbari ambayo yanapangwa katika DRC, kwa sababu kuyatambua unakwenda sambamba na uwajibikaji wa kuingilia kati na kuyazuia ," alisema Biruta.

Aliongeza kwamba wanakwepa uwajibikaji, lakini wataendelea kuwakumbusha.

Hali hiyo inakuja wakati DRC, ikiendelea kuishutumu Rwanda kuwaunga mkono waasi wa M23, katika mzozo wa kivita unaoendelea kwa muda wa muongo mmoja mashariki mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, Rwanda imekanusha madai hayo yanayotolewa mara kwa mara.

Serikali ya Rwanda pia imeishutumu DRC kwa kuwaunga mkono waasi wa kundi la Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR), ambalo linajumuisha washukiwa wa mauaji ya kimbari ya Rwanda ya mwaka 1994.

Mwezi Desemba mwaka jana wavuti wa gazeti la serikali ya Rwanda ulisema kauli za chuki na mauaji yanayowalenga Watutsi na raia Wacongo wanaozungumza Kinyarwanda yanaweza kuwa kiashiria cha uwezekano wa mauaji ya kimbari.

**BBC**



Wanamgambo wa kundi la waasi la M23 wakiwa katika harakati zao mashariki mwa DRC, ambako mauaji ya watu 15 yalifanyika juzi. **PICHA:LFP**

# Upinzani Zambia waikemea Marekani

**LUSAKA,** ZAMBIA

CHAMA kikuu cha upinzani nchini Zambia, Patriotic Front (PF), kimeelezea wasiwasi wake kwamba Marekani inasukuma ajenda ya mapenzi ya jinsia moja katika nchi hiyo.

Kiongozi wa chama hicho, Given Lubinda, alitoa maoni hayo baada ya Rais wa Marekani Joe Biden, kuelekeza kuendeleza usawa kwa watu wa LGBT.

"Kama Patriotic Front, tunawasihi Wazambia kutoruhusu Marekani kulazimisha maadili yake nchini mwetu. Ni lazima tujitetee," alisema Lubinda.

Alisema kuwa uhusiano wa nchi hizo mbili usiegemee misaada ya Marekani ambayo inafungamana na haki za LGBTQ.

Lubinda alisema Zambia inaweza kulazimika kupitia upya uhusiano wake na Marekani.

Aliwataka Wazambia kutotupilia mbali kanuni zao, maadili ya kitaifa, msimamo wa kidini na kitamaduni ili kuwafurahisha Wamarekani.

Matamshi ya chama hicho yanakuja siku chache kabla ya ziara iliyopangwa ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, nchini humo wiki ijayo.

Mnamo tarehe 14 Machi, Rais Hakainde Hichilema aliahidi kudumisha sheria za Zambia ambazo zinaharamisha jamii ya LGBTQ na kutaja madai ya uwongo kwamba serikali yake inaunga mkono haki za watu wa mapenzi ya jinsia moja.

Katika ziara yake ya siku tisa barani Afrika itakayoanza Machi 26, Harris pia anatarajiwa kuzuru Ghana na Tanzania, ambako pia mahusiano ya watu wa jinsia moja ni haramu .

Nchini Uganda, wabunge waliidhinisha muswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja ambao unaweka adhabu kali kwa yeyote anayejihusisha na jamii hiyo

**BBC**

## Malema aahidi kumlinda Putin

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

CHAMA cha Economic Freedom Fighters cha Afrika Kusini (EFF), kinachoongozwa na Julius Malema, kimeahidi kumlinda Rais wa Russia, Vladimir Putin, wakati atakapokwenda nchini humo.

Kauli hiyo inatokana na hatua ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kutoa hati ya kumkamata kwa makosa mbalimbali ya kivita.

Mahakama ya ICC, ambayo Afrika Kusini ni mwanachama, imemshutumu Putin kwa uhalifu wa kivita, ambao ni pamoja na utekaji nyara wa watoto wa Ukraine.

Putin amealikwa kwenda Afrika Kusini kuhudhuria mkutano wa kilele wa Brics unaojumuisha Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini, utakaofanyika mwezi Agosti. Malema alisema hakuna mtu atakayemkamata Putin akiwa Afrika Kusini, nchi ambayo Russia ilichukua jukumu kubwa la kuunga mkono mapambano ya uhuru.

Malema alisema kuwa serikali ya Afrika Kusini haipaswi kukubali shinikizo kutoka kwa ICC, ambayo aliishutumu kwa unafiki. "Putin anakaribishwa hapa. Hakuna atakayemkamata Putin. Ikibidi tutaenda kumchukua uwanja wa ndege hadi kwenye mikutano yake. Atahutubia, atamaliza mikutano yake yote, na tutamrudisha uwanja wa ndege akiwa salama, " alisema Malema.

"Tunawajua marafiki zetu. Tunawajua watu waliotukomboa. Tunawajua watu waliotuunga mkono," aliongeza.

Afrika Kusini ina uhusiano wa karibu wa kidiplomasia na Russia licha ya kulaaniwa na nchi za Magharibi. Mwezi uliopita, jeshi lake la wanamaji lilifanya mazoezi ya pamoja na vikosi vya Russia katika pwani ya Afrika Kusini.

## Pierre Bemba ateuliwa waziri

**KINSHASA**, DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, amemteua makamu wa zamani wa rais Jean Pierre Bemba, kuwa waziri wa ulinzi.

Rais Tshisekedi amefanya uteuzi huo katika mabadiliko makubwa ya baraza la mawaziri.

Pierre Bemba kiongozi wa zamani wa wanamgambo aliyehukumiwa kifungo cha miaka 10 na mahakama ya kimataifa ya makosa ya uhalifu (ICC) kwa madai ya uhalifu wa kivita, anakuwa miongoni mwa wateule katika baraza la mawaziri 57.

Msemaji wa serikali alisema uteuzi wake ulikuwa ni wa muhimu na wa dharura, katika tangazo alilolitoa kupitia televisheni ya taifa juzi usiku.

Bemba alikuwa makamu wa rais kati ya mwaka 2003 hadi 2006.

Mabadiliko haya ya mawaziri ambayo ni makubwa zaidi, yanafanyika kabla ya uchaguzi wa rais unaotarajiwa kufanyika Desemba 20 mwaka huu.

Rais Tshisekedi huenda akawania awamu ya pili.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Spora Manase Mbowe** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1324-0060** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Harambee Secondary School mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/426592/2022.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**OSCAR RWESSA ZABLON,** MKAZI WA KIBADA, KIGAMBONI, DAR ES SALAAM, AMEPOTEZA PASSPORT YAKE YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TARR36017** ILIYOTOLEWA TAREHE 12/03/2021. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **DAR/KIG/RB/521313/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**GETRUDE SIAYAKO ALOYCE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S0729-0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MSOLWA ST. GASPAR BERTONI SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/DAR/RB/108074/2023.**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha: MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 35/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**NOVATY RUGEMELEZA WA AREA SIX**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA PATRICIA KAYOKA KASWAHILI**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 / Mwezi 04 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 03 mwaka 2023**

HAKIMU

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 481/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ABDALLAH SAIDI BORI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MOHAMED ABDALLAH BORI**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 04 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi 03 Mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YEHOVANICE ELIAMRINGI MACHANG'U** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 791 CER.** Chassis No **KE7KEFPK006177.** Engine NO **162FMJC5119212.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/108179/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YEHOVANICE ELIAMRINGI MACHANG'U** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki – Bajaji Boxer yenye namba za usajili **MC 178 AED.** Chassis No **MD2A21BZ6DWE30924.** Engine **NO PFZWDC20986.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/108304/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YEHOVANICE ELIAMRINGI MACHANG'U** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki – **Bajaji Boxer** yenye namba za usajili **MC 557 BRF.** Chassis No **MD2A21BZ3HWM51068.** Engine NO **PFZWHM73778.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/108296/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YEHOVANICE ELIAMRINGI MACHANG'U** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki – **Bajaji Boxer** yenye namba za usajili **MC 644 BFW.** Chassis No **MD2A21BZ6GWM62502.** Engine NO **PFZWGM27475** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/108293/2023.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*
***0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-1




**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Ndugu wanahabari na wananchi kwa ujumla, kwa masikitiko, Jeshi la Polisi linatangaza kuwa maeneo ya Kinondoni Msisiri umeokotwa mwili wa mtu ukiwa umekatwakatwa vipande na kutumbukizwa kwenye kiroba.

Na nikisema mwili, sina maana kuwa ulikuwa mwili mzima, bali kilichokutwa na vipande vipande vya mwili ambavyo vilikatwakatwa na mtu huyo katili na kuwekwa kwenye kiroba.

Inavyoonekana kiroba hicho kimewekwa hapo usiku au alfajiri na mmoja wa vijana wanaotupa taka, au wanaookota chupa ambazo huwa wanakwenda kuziuza.

Uchunguzi wa awali wa madaktari unasema mwili huo ni wa mtu mmoja na wala si wawili au watatu kama mwanzo ilivyohisiwa, lakini pia marehemu ni mwanamke."

Ilikuwa ni sauti nzito, yenye huzuni ya Kamanda wa Polisi Mkoa aliyekuwa akiwahabarisha wananchi juu ya tukio hilo.

"Kusema kweli tukio hili limetia simanzi, na limeleta taharuki kubwa si kwa wananchi wa kanda yetu, bali hata Watanzania kwa ujumla.

Ninawahakikishia wananchi jeshi letu lipo imara, limeshaanza uchunguzi wa kujua mwanamke huyu ni nani. Ametoka wapi. Alikuwa anakwenda wapi na imekuwaje. Pia wahusika wote waliofanya hivi, tunawakikishia kuwa watapatikana na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria, na kila kitu kitakachokuwa kinaendelea hatua kwa hatua tutawahabarisha, nawaomba tuwe watulivu," alisema Kamanda huyo.

Lilikuwa ni moja ya tukio kubwa na la kuhuzunisha ambalo nalo 'lilitrendi' sana kwenye mitandao ya kijamii. Kila mmoja alikuwa akisema lake.

Hata hivyo lilikuwa ni moja kati ya matukio mengi ambayo kwa sasa yanajitokeza sana kwenye jamii, na yanasahaulika kirahisi kwa sababu kila baada ya siku mbili tatu linatokea lingine la kushangaza, kustaajabisha na kusikitisha.

Imekuwa si ajabu kwa sasa ukiamka kukuta mama amemuua mjukuu wake, mtoto wake wa kambo, na hata wa kumzaa mwenyewe kwa sababu mbalimbali.

Ukiamka utasikia mtoto kamuua baba yake au mama yake ili apate urithi. Kama vile haitoshi, unakutana na habari ya mke kumchoma moto mumewe kwa wivu, au mume kumuua mkewe baada ya kumfumania.

Kali kuliko yote, siku hizi wala si ajabu kusikia eti mwanaume kamuua mchepuko wake, tena utakuta yeye ana mke na huo mchepuko nao una mumewe. Huku ndiko ambako tumefikia.

**"Mhh jamani Vingunguti na Kinondoni wapi na wapi?" alishusha ujumbe mfupi kwenye mtandao wa kijamii msomaji mmoja baada ya habari hiyo kutoka na kuthibitishwa na polisi.**

Habari 'zilizotrendi' kesho yake ni kwamba mwanamke ambaye viungo vyake viliokotwa Kinondoni Msisiri ni mkazi wa Vingunguti, Dar es Salaam. "Mhh jamani Vingunguti na Kinondoni wapi na wapi?" alishusha ujumbe mfupi kwenye mtandao wa kijamii msomaji mmoja baada ya habari hiyo kutoka na kuthibitishwa na polisi.

Wanahabari kama kawaida yao walikwenda kwenye msiba ambapo mjomba wa marehemu aliulizwa maswali kadhaa, na hakukaa kimya akaeleza jinsi ilivyokuwa.

"Naitwa Peter Voley, ni mjomba wa marehemu Tessy. Taarifa ambazo tulizipata awali ni kwamba alitoweka nyumbani kwa siku tatu, na siku ya nne ndiyo tukapata taarifa kuwa kuna mwili umeokotwa Kinondoni, lakini umekatwatwa viungo kila kitu kwake halafu umefungwa kwenye kiroba. Tukaitana ndugu tukawahi kwenye Hospitali ya Taifa, Muhimbili ili kuutambua na kweli tulipofika tukakuta ndiyo wenyewe, japo ilibidi tufanye kazi ya ziada kwa sababu viungo vimetenganishwa," alisema.

Akaulizwa kama anahisi mauaji hayo yametokana na nini, au kuna siku alishawahi kuwaambia kuwa amegombana na mtu, Peter akajibu kuwa hawezi kufahamu.

"Tessy ni mfanyabiashara, ana maduka ya nguo Ukonga na Buguruni, huwezi kujua, lakini sidhani kama inaweza kuwa hivyo. Ila nikiri tu siyo kifo cha kawaida, inabidi uchunguzi wa kina ufanyike."

Waandishi wakamuuliza mume wa marehemu, akawajibu kuwa alikuwa amezirai, na sasa fahamu ndiyo zinamrudia, hivyo hawezi kuongea hivyo wamuache apumzike.

Wakati amepotea kwa siku hizo tatu mumewe hakuwepo. Mumewe ni mfanyakazi, alikuwa Dodoma, mara nyingi hurejea wikiendi, mume wiki nzima anakuwa Dodoma na mke Dar es Salaam, Ijumaa anarejea, na Jumapili anarudi Dodoma. Unajua alipotoweka siku ile ya kwanza mumewe alikasirika sana, unajua tena mambo ya wivu, lakini siku ya pili akanywea, akaona hii sasa siyo kawaida. Bahati nzuri siku ya pili ilikuwa Ijumaa, akatuagiza tu kwanza tukatoe taarifa polisi, siku ya ya tatu bado tulikuwa tunahangaika huku na huko, siku yake haipatikani, kila tunapoenda hata kwenye biashara zake hayupo hadi tulipopata hiyo taarifa. Naweza kusema sisi ndugu wa marehemu tumefiwa, lakini aliyepata pigo zaidi ni mumewe. Kwanza ni jinsi alivyoishi kwa amani na mkewe. Aina ya kifo cha mkewe pia kimezidi kumtia simanzi, sijui baada ya hapo ataishi vipi. Tunaomba tu Jeshi la Polisi kufanya kila njia kuwakamata watu hawa."

Maongezi ya mjomba Peter yalichapishwa kwenye magazeti pamoja na kwenye mitandao ya kijamii. Watu wakaendelea kuhuzunika. Wakitaka wauaji watafutwe haraka ili sheria ichukue mkondo wake.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# GEITA GOLD FC YAJIPANGA KUISIMAMAMISHA YANGA FA

Na Shufaa Lyimo

KIKOSI cha Geita Gold FC kinaendelea na mazoezi maalumu ya kuimarisha timu yao kuelekea mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC), utakaochezwa Aprili 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Geita Gold itawafuata Yanga ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi iliyopita ya mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kulazimisha sare katika mchezo wa kwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Geita Gold, Mathius Wandiba, alisema wanawaandaa wachezaji wao kiufundi na kisaikolojia kwa sababu wanahitaji kushinda na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Wandiba alisema anafurahi kuona ushindani ni mkubwa katika mazoezi ya timu hiyo huku nyota hao wakijiimarisha kimwili.

"Tumewaandaa wachezaji wetu vizuri kuelekea katika mchezo huo, tunafahamu utakuwa mgumu na wenye ushindani, tunajiwinda ili kutimiza lengo la kuingia hatua ya nusu fainali," alisema Wandiba.

Kocha huyo alisema makosa ambayo waliyaona katika michezo iliyopita wanaendelea kuyafanyia marekebisho na kuwasisitiza wachezaji kuongeza umakini wanapokaribia lango la wapinzani.

Alisema hawahofii kukutana na Yanga ambayo itaingia katika mechi hiyo ikiwa na rekodi ya matokeo bora kwenye michezo yake ya kimataifa ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Hatuna wasi wasi kukutana na Yanga, kufanya vizuri katika michezo ya kimataifa si kigezo cha kuwaogopa, hii ni michuano mingine ambayo ina mbinu na kanuni tofauti," Wandiba aliongeza.

Amewataka mashabiki wao waliopo Dar es Salaam kujipanga kujitokeza kushangilia kwa sababu wamepanga kutimiza malengo yao ya kushiriki michuano ya kimataifa katika msimu ujao.




Mlezi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, Fatema Dewji (kushoto), akiwapatia wachezaji wa timu hiyo zawadi ya televisheni ya kisasa kwa ajili ya kuangalia vipindi mbalimbali kama sehemu ya kuukaribisha mwezi wa Ramadhani. **PICHA: SIMBA SC**

# Gofu vijana kuchuana Uganda

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya gofu kwa wachezaji wenye umri kati ya miaka 14 na 18 ya Afrika Mashariki yamepangwa kufanyika Aprili, mwaka huu jijini Kampala, Uganda imeelezwa.

Lengo la michuano hiyo ni kupata wachezaji watakaoziwakilisha nchi zao katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Enock Magile, alisema katika mashindano hayo Tanzania itawakilishwa na wachezaji nane.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano ya vijana yanaendelea vyema, tunasubiri wanafunzi waanze likizo ya Sikukuu ya Pasaka ili waingie kambini kwa ajili ya kujifua," alisema Magile.

Katibu huyo alisema wachezaji watano watatoka katika Klabu ya Lugalo, Gymkhana mmoja na klabu za mikoa Kilimanjaro na Arusha kila moja itatua mchezaji mmoja.

"Tunatafuta wadhamini watakaotusaidia fedha kwa ajili ya safari ya kwenda katika mashindano pamoja na kulipa posho za wachezaji," Magile aliongeza.

## Azam FC, KMC kujipima ubavu

Na Adam Fungamwango

WAKATI Ligi Kuu Bara imesimama kupisha kalenda ya mechi za kimataifa, Azam FC na KMC zinatarajia kukutana katika mchezo wa kirafiki utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Azam FC imesema baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya JKU ya Zanzibar, wameamua kujiimarisha kwa kuendelea kujipima nguvu.

Awali Azam walitarajia kujipima na vigogo wa Kenya, Gor Mahia lakini mchezo huo wa kirafiki wa kimataifa ulivunjika kutokana na machafuko ya kisiasa yanayoendelea kwa majirani zao.

Wakati huo huo, KMC inayonolewa na Thiery Hitimana imeifunga bila huruma Dar City inayoshiriki Ligi ya Championship mabao 8-0 katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana asubuhi.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi 47 na katika hatua ya robo fainali ya Kombe la FA itacheza dhidi ya Mtibwa Sugar huku KMC yenyewe bado haiko pazuri inahitaji kujiimarisha ili ijinasue mkiani.

## Bosi ZFF awafunda viongozi wa wilaya

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

VIONGOZI waliochaguliwa katika vyama vya soka vya wilaya zote za Zanzibar wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kutimiza malengo ya kunyanyua soka la visiwani hapa, imeelezwa.

Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Abdul-Latif Ali Yasin, aliliambia gazeti hili amewataka viongozi hao waliochaguliwa hivi karibuni kufanya kazi kwa weledi na ili kuleta ufanisi katika kuendeleza mchezo huo.

Yasin alisema ushirikiano uliopo bado si mzuri na hautaweza kusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa na ZFF katika kusimamia na kuliendeleza soka la Zanzibar.

"Tunahitaji kupiga hatua katika ngazi zote, tunavikumbusha vyama vyote katika wilaya 11 za Zanzibar kufanya kazi kwa karibu, kujenga mahusiano yatakayoleta mafanikio makubwa katika soka letu," alisema Yasin.

Rais huyo aliahidi kuendelea na utaratibu wa kuvitembelea vyama hivyo huku pia akiwakumbusha viongozi kuwa waadilifu na kutunza siri za ofisi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MADRID YAMTIZAMA HAALAND**
REAL Madrid wameanzisha tena 'Operesheni Haaland' kwa nia ya kumsajili mshambuliaji mahiri wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22 kutoka Manchester City kwa mwaka 2024, wakati kipengele cha kutolewa katika mkataba wake cha hadi euro 240 kitakapoanza kutumika. ***(AS)***

**TUCHEL ANUKIA BAYERN**
BAYERN Munich wameamua kumfukuza kocha, Julian Nagelsmann, mwenye umri wa miaka 35, huku Mjerumani mwenzake na kocha wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel akiwa mgombea anayeongoza kuchukua nafasi yake. ***(Bild)***

**NAGELSMAN KUMRITHI CONTE**
TOTTENHAM Hotspur inaweza kumgeukia, Julian Nagelsmann kama mbadala wa Mtaliano, Antonio Conte, mwenye umri wa miaka 53, ambaye anaonekana kutaka kuondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuua England. ***(Soccer.London)***

**ILING-JUNIOR AINGIA SOKONI**
CHELSEA, Manchester City na Newcastle United zinafikiria kumnunua winga wa Juventus mwenye umri wa miaka 19, Samuel Iling-Junior ifikapo msimu wa joto. ***(90 min)***

**RASHFORD AWEKA MSIMAMO**
MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 25, hatasita kusaini mkataba mpya na Manchester United hadi wamiliki wapya wa klabu hiyo watakapothibitishwa. ***(Sun)***

**AKHOMACH AGEUKA LULU**
ARSENAL wameungana na Leeds United, AC Milan na Sevilla katika mbio za kuwania huduma ya mchezaji wa kimataifa wa Hispania na Barcelona mwenye umri wa miaka 18, Ilias Akhomach. ***(Sport)***

**LIVERPOOL, UNITED VITANI**
LIVERPOOL inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester United kupata huduma za gwiji wa kuajiri, Paul Mitchell, mwenye umri wa miaka 41 ambaye ataondoka Monaco msimu huu wa joto. ***(Mirror)***

**CITY, PSG ZAMWANIA KINDA**
KLABU ya Manchester City inafanyia kazi mpango wa kumnunua beki wa kati wa Hajduk Split, Luka Vuskovic, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Paris St-Germain kumnunua raia huyo wa Croatia mwenye umri wa miaka 16. ***(Fabrizio Romano)***

**GIOVANI ANUKIA ENGLAND**
EVERTON imejiunga na Newcastle United katika kufikiria kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Giovani, mwenye umri wa miaka 19 anayechezea Palmeiras. ***(ESPN Brazil)***

**EVERTON YAMTAKA MAUPAY**
EVERTON itamnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Neal Maupay, mwenye umri wa miaka 26 kwa ajili ya kuuzwa msimu wa joto. ***(Football Insider)***

**MESSI AISOGELEA BARCA**
NAFASI ya fowadi wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35 kuondoka Paris St-Germain na kujiunga na klabu yake ya zamani ya Barcelona inaongezeka. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AFUNGA MABAO 800

●●●Ndiye mshambuliaji anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi Barca lakini...

**BUENOS AIRES, Argentina**

LIONEL Messi alifunga bao lake la 800 tangu aanze kucheza soka la kiwango cha juu wakati Argentina ilipoifunga Panama mabao 2-0 katika mechi yao ya kwanza tangu waliposhinda Kombe la Dunia mwaka jana.

Fowadi huyo wa Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 35 anakuwa mchezaji wa pili kufikia hatua hiyo baada ya Cristiano Ronaldo.

Idadi ya mabao ya Messi ni pamoja na mabao 672 katika misimu 17 akiwa na Barcelona na 29 akiwa na PSG.

Pia ana mabao 99 ya kimataifa, huku mawili akifunga kwenye fainali ya Kombe la Dunia.

Nahodha huyo wa Argentina alifunga kwa faulo dakika ya 89 kwenye Uwanja wa Monumental de Nunez mjini Buenos Aires baada ya lile la kwanza lililofungwa na Thiago Almada dakika 11.

Messi atapata fursa ya kufunga bao lake la 100 la kimataifa wakati Argentina itakapocheza na Curacao hapo Jumanne.

Ni hatua nyingine katika maisha yake ya ajabu ambapo ameshinda takribani kila taji kuu, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne, mataji 10 ya LaLiga, Copa America na, hatimaye Desemba mwaka jana alitwaa Kombe la Dunia.

Akiwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote, Messi ameshinda Ballon d'Or mara saba - tuzo ya mchezaji bora wa mwaka katika soka ya Ulaya - akimzidi mbili mpinzani wake wa karibu, Ronaldo.

Shindano pekee kubwa ambalo Messi amecheza lakini ameshindwa kushinda hadi sasa ni Kombe la Ufaransa.

Kunyakua mataji 35 kwa Messi akiwa na Barcelona, ambaye alijiunga naye akiwa na umri wa miaka 13, kunamfanya kuwa mchezaji aliyepambwa zaidi katika historia ya klabu hiyo ya Hispania na bila ya kustaajabisha anashikilia rekodi za kufunga mabao mengi zaidi kwa Barca (778).

Pia amefunga mabao mengi zaidi (474) na kutoa pasi nyingi za mabao (192) kuliko mchezaji yeyote aliyecheza LaLiga na ana rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja katika ligi kuu ya Hispania - mabao 50 katika mechi 37 msimu wa 2011-12.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,093,3

MECHI KALI

SPAIN
VERSUS
NORWAY

1 | 1.40
X | 4.64
2 | 8.20

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TUCHEL ANUKIA BAYERN, NAGELSMANN ATIMULIWA

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich imemfuta kazi kocha wake, Julian Nagelsmann na sasa Thomas Tuchel yuko mbioni kuchukua nafasi hiyo.

Ingawa haijathibitishwa rasmi na klabu hiyo ya Ujerumani, ripoti zilizoenea jana zilisema Nagelsmann amefukuzwa kazi.

Bayern wanashika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, pointi moja nyuma ya Borussia Dortmund, na ni mmoja wa makocha wa zamani wa wapinzani wao ambaye anapendekezwa kuchukua nafasi ya Nagelsmann.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Fabrizio Romano, Tuchel - ambaye alitimuliwa Chelsea Septemba, mwaka jana tayari amekubali kuwa kocha mpya wa Bayern.

Mechi ya kwanza ya Tuchel itakuwa dhidi ya timu yake ya zamani Dortmund itakayochezwa Aprili Mosi, mwaka huu.

Bayern itacheza na Manchester City katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nagelsmann, wakati huo huo, ana uhakika wa kuhusishwa na fursa nyingi za kazi za hali ya juu.

# Mbappe afunguka kuhusu Griezmann

**PARIS, Ufaransa**

JUKUMU la Kylian Mbappe kama nahodha wa Ufaransa litakuwa ni kuunganisha kizazi cha zamani na kipya cha wachezaji katika kikosi, fowadi huyo wa Paris Saint-Germain alisema katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari tangu kupata kazi hiyo.

Mbappe aliteuliwa kuwa nahodha wa Ufaransa akichukua nafasi ya Hugo Lloris, siku ya Jumanne baada ya mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 36 kutangaza kustaafu soka la kimataifa tangu Januari.

Mbappe mwenye umri wa miaka 24 alipewa kazi maalum na Kocha, Didier Deschamps.

"Anataka niwe mtu wa kuunganisha, kuleta timu yake pamoja nami. Mimi ndiye kiungo kati ya vizazi," alisema Mbappe.




Mbappe alisema Nahodha Msaidizi, Antoine Griezmann, amesikitishwa na uamuzi huo. Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa mchezaji wa muda mrefu wa Deschamps, akiichezea nchi yake kwa mara ya kwanza mwaka 2014.

"Pengine ndiye mchezaji muhimu zaidi wakati wa zama za Deschamps. Mimi si kiongozi wake wa ngazi ya juu.

Mechi ya kwanza ya Mbappe kama nahodha ilikuwa jana Ijumaa wakati Ufaransa ilipocheza na Uholanzi kwenye Uwanja wa Stade de France kuwania kufuzu Euro 2024.

395,265/-

# MKONGOMANI ANUKIA UFUNGAJI LIGI YA CHAMPIONSHIP 2022/23

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI katika Ligi Kuu Tanzania Bara, straika wa Yanga, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Fiston Mayele akiongoza kwenye orodha ya ufungaji, Mkongomani mwenzake, Ngoyi wa Ngoyi Fabrice 'anakimbiza' kwenye Ligi ya Championship.

Mayele amepachika mabao 15 wakati Ngoyi wa Ngoyi anayeitumikia Kitayosce ya Tabora ameshafunga magoli 13 mpaka sasa.

Kitayosce iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo lakini nafasi ya pili katika ufungaji inafuatiwa na straika Mtanzania anayeichezea JKT Tanzania, vinara wa ligi hiyo amefunga mabao 11.

Adam Uledi wa Kengold FC anafuatia akiwa na mabao nane na Deogratius Kulwa anayeichezea Pamba FC, akifunga mabao saba.

Wachezaji waliofunga mabao sita kila mmoja ni Emmanuel Mpuka wa Kengold FC, Eliya Ashley (JKT Tanzania), Francis Ndala (Copco), Jeremiah Joseph na John Elius wote wa Mashujaa.

JKT Tanzania inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 53, ikifuatiwa na Kitayosce yenye pointi 46, Pamba FC nafasi ya tatu kwa pointi zake 44 na Mashujaa inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi 38 huku Fountain Gate iliyopo nafasi ya tano imejikusanyia pointi 37.

Mbeya Kwanza ya Mbeya iko katika nafasi ya sita ikiwa na pointi 34, na tayari timu zote zimeshacheza michezo 22.

Timu mbili zitakazomaliza nafasi ya kwanza zitapanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.



Wachezaji wa Ihefu SC ya Mbarali, Mbeya wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuwafuata Simba katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa Aprili 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Stars yaichapa Uganda

INATOKA UK. 24

akiwa hayupo langoni.

Kipindi cha pili Stars ilionekana kuchangamka hasa baada ya kuingia kwa Abdul Suleiman Sopu aliyechukua nafasi ya Said Khamis na baadaye Feisal Salum aliyembadili Mudathir Yahaya.

Kabla ya bao hilo, Sopu alikaribia kuiandikia Stars bao dakika ya 64, alipomlamba chenga, Ochaya na kuachia kombora kali lililopanguliwa kwa ustadi na Magoola.

Hata hivyo, dakika 10 za mwisho, Waganda walionekana kuamka tena wakifanya mashambulizi mfululizo kupitia kwa wachezaji wao waliowaingia kipindi cha pili, Isma Mugulusi, Allan Okello na Richard Basangwa, lakini mabeki wa Stars, Job Novatus ambaye jana alicheza beki ya kulia, Bakari Mwamnyeto, na Ibrahim Abdallah 'Bacca', chini ya kipa Manula, walikaa imara kuzuia hatari zote.

Timu hizo zitarudiana Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni raundi ya nne ya michuano hiyo.

## Simba SC, Yanga

INATOKA UK. 24

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji wote ambao hawako katika timu za taifa wameanza kujifua kujiandaa na mchezo huo wa kukamilisha ratiba lakini muhimu kuelekea hatua inayofuata.

"Tunatambua mchezo utakuwa mgumu sana kwa ubora wa wapinzani wetu, hatutaenda kinyonge katika mechi hiyo, kwa sababu tunahitaji kutafuta angalau alama moja," alisema Ahmed.

Aliongeza kama ilivyo kawaida yao, wametanguliza ofisa ambaye anakwenda kuandaa mazingira bora ya mahali timu itakapofikia na maandalizi mengine muhimu ambayo wanalenga kupata matokeo chanya.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/03/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Northampton Town | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 02. 25/03/23 | 18:00 | Peterborough United vs Derby County | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 03. 25/03/23 | 18:15 | Racing Santander vs Levante UD | 3.45 | 3.00 | 2.15 |
| 04. 25/03/23 | 18:15 | UD Ibiza vs Burgos CF | 2.33 | 2.80 | 3.30 |
| 05. 25/03/23 | 23:00 | Bogota FC vs Tigres FC | 2.27 | 2.85 | 2.90 |
| 06. 25/03/23 | 23:30 | Portland Timbers vs Los Angeles Galaxy | 2.14 | 3.30 | 2.70 |
| 07. 26/03/23 | 02:30 | DC United vs New England Revolution | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 08. 26/03/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 2.39 | 3.00 | 2.60 |
| 09. 26/03/23 | 02:30 | Columbus Crew vs Atlanta United FC | 2.40 | 3.10 | 2.50 |
| 10. 26/03/23 | 03:30 | Houston Dynamo vs New York City FC | 2.44 | 3.10 | 2.45 |
| 11. 26/03/23 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Seattle Sounders | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 12. 26/03/23 | 04:05 | CF Correcaminos UAT vs CD Mineros de Zacatecas | 2.16 | 2.95 | 2.95 |
| 13. 26/03/23 | 06:05 | Pumas de Tabasco vs Raya2 Expansion | 2.49 | 2.95 | 2.49 |
| 14. 26/03/23 | 08:00 | Iwaki FC vs Machida Zelvia | 2.50 | 2.95 | 2.47 |
| 15. 26/03/23 | 15:30 | FC Dordrecht vs Helmond Sport | 2.47 | 3.15 | 2.39 |
| 16. 26/03/23 | 17:15 | SD Ponferradina vs CD Mirandes | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 17. 26/03/23 | 17:15 | Real Zaragoza vs Albacete Balompie | 2.10 | 3.00 | 3.50 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 25/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1658 | Tuzlaspor vs Goeztepe | 2.66 | 3.22 | 2.36 |
| 13:30 | 5455 | Keciorengucu vs Genclerbirligi | 1.75 | 3.55 | 3.91 |
| 15:00 | 4070 | Frederikssund vs BK Avarta | 3.32 | 3.74 | 1.88 |
| 15:30 | 5621 | Slough Town vs Ebbsfleet | 5.81 | 4.26 | 1.44 |
| 16:00 | 4016 | Altay vs Manisa BBSK | 3.12 | 3.27 | 2.07 |
| 16:30 | 1711 | Renate vs Padova | 3.14 | 3.14 | 2.31 |
| 16:30 | 5208 | Scheveningen vs FC Volendam | 1.71 | 3.55 | 3.65 |
| 16:30 | 5663 | Persebaya Surabaya vs PS Tni | 1.80 | 3.48 | 3.74 |
| 17:00 | 1167 | Znojmo vs FC Slovan Rosice | 2.14 | 3.73 | 2.75 |
| 17:00 | 1666 | Scotland vs Cyprus | 1.30 | 5.31 | 10.83 |
| 17:00 | 3575 | Carmarthen Town AFC vs Goytre United | 1.45 | 4.42 | 5.14 |
| 17:30 | 3940 | The New Saints vs Cardiff Met Uni. | 1.15 | 6.42 | 13.46 |
| 17:30 | 4043 | Barry Town FC vs Pontardawe Town FC | 1.18 | 6.16 | 9.86 |
| 17:30 | 5780 | Penybont vs Bala Town | 2.12 | 3.32 | 3.06 |
| 18:00 | 1021 | MK Dons vs Morecambe | 1.75 | 3.52 | 4.43 |
| 18:00 | 1884 | Peterborough vs Derby | 2.52 | 3.38 | 2.58 |
| 18:00 | 2918 | Juventus Zurich vs Breitenrain | 4.62 | 3.95 | 1.56 |
| 18:00 | 3235 | Boreham Wood vs Eastleigh | 1.97 | 3.42 | 3.52 |
| 18:00 | 3748 | Exeter vs Accrington | 1.72 | 3.64 | 4.45 |
| 18:00 | 4046 | Annan Athletic vs Stranraer | 1.77 | 3.60 | 3.75 |
| 18:00 | 4075 | Fleetwood Town vs incoln | 2.33 | 3.07 | 3.07 |
| 18:00 | 4305 | Doncaster vs Northampton | 3.36 | 3.16 | 2.06 |
| 18:00 | 4403 | Warrenpoint vs Dergview | 1.49 | 4.22 | 4.94 |
| 18:00 | 4697 | Coleraine FC vs Larne | 3.13 | 2.98 | 2.20 |
| 18:00 | 5366 | Stenhousemuir vs Forfar Athletic | 2.07 | 3.38 | 3.02 |
| 18:00 | 5447 | Barrow vs AFC Wimbledon | 2.09 | 3.08 | 3.38 |
| 18:00 | 5634 | Yate Town vs Bracknell Town | 6.63 | 4.97 | 1.34 |
| 18:00 | 5853 | Stirling vs Dumbarton | 1.91 | 3.44 | 3.39 |
| 18:00 | 5947 | Knockbreda vs Institute | 2.98 | 3.64 | 2.00 |
| 18:30 | 5984 | CD Constancia vs SD Portmany | 1.61 | 3.40 | 5.15 |
| 19:30 | 4243 | Teungueth vs Cneps | 1.56 | 3.32 | 6.43 |
| 19:30 | 5160 | UD Collerense vs Santanyi | 3.13 | 2.97 | 2.20 |
| 20:00 | 4210 | Sligo Rovers vs Treaty United | 1.45 | 4.09 | 6.01 |
| 20:00 | 5014 | Belarus vs Switzerland | 12.00 | 5.67 | 1.27 |
| 20:00 | 5728 | Armenia vs Turkey | 6.96 | 4.24 | 1.49 |
| 20:00 | 5787 | Israel vs Kosovo | 2.00 | 3.42 | 3.90 |
| 20:30 | 5501 | Alaves vs Tenerife | 1.91 | 3.00 | 4.30 |
| 21:00 | 2462 | AL Arabi vs AL-Rams | 1.70 | 3.60 | 4.11 |
| 21:00 | 3801 | Al-Thaid vs Fursan Hispania FC | 1.31 | 4.71 | 7.38 |
| 21:00 | 4178 | United Arab Emirates vs Tajikistan | 1.40 | 4.83 | 7.30 |
| 21:00 | 4581 | Bermuda vs Guyana | 2.19 | 3.22 | 3.01 |
| 22:30 | 3209 | Turks And Caicos Islands vs Virgin Islands, U.S | 2.21 | 3.43 | 2.81 |
| 22:45 | 2317 | Spain vs Norway | 1.40 | 4.64 | 8.20 |
| 22:45 | 2393 | Andorra vs Romania | 13.00 | 5.63 | 1.26 |
| 22:45 | 4528 | Croatia vs Wales | 1.65 | 3.76 | 5.27 |
| 22:45 | 4871 | Germany vs Peru | 1.34 | 5.15 | 8.36 |
| 23:00 | 4282 | Detroit City FC vs Indy Eleven | 1.79 | 3.53 | 3.89 |
| 23:00 | 4471 | Sint Maarten vs Bonaire | 2.96 | 3.48 | 2.11 |
| 23:00 | 4724 | AD Cofutpa vs ADR Jicaral | 3.16 | 3.26 | 2.10 |
| 23:30 | 2131 | Portland Timbers vs LA Galaxy | 2.30 | 3.41 | 2.93 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Machi 25, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Messi afunga mabao 800



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakipiga picha ya 'Selfie' baada ya mshambuliaji, Simon Msuva (katikati aliyeshika simu), kufunga bao pekee katika mechi hiyo dhidi ya Uganda (Cranes) ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Suez Canal mjini Ismailia, Misri jana. **PICHA: TFF**

# STARS YAICHAPA UGANDA

## ●●●Bao pekee lililofungwa na Msuva larejesha matumaini ya kufuzu AFCON...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na winga, Simon Msuva, anayeichezea klabu ya Al-Qadsiah ya Saudi Arabia limeiwezesha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uganda (Cranes), katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali ya Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Suez Canal mjini Ismailia, Misri jana.

Uganda iliutumia uwanja huo kutokana na viwanja vya nchini mwao kutokidhi vigezo vya michuano hiyo ambayo fainali zake zitafanyika mwakani huko Ivory Coast.

Msuva aliukwamisha mpira huo wavuni akiandika bao lililokuwa likisubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka wa Tanzania dakika ya 68.

Mpira ulianzia katikati ya uwanja kwa Mzamiru Yassin, ambaye alipiga mpira mrefu kwenye wingi ya kulia, uliomkuta Dickson Job ambaye alipiga krosi chonganishi, akiwa katikati ya walinzi, winga huyo aliwazidi maarifa na kuukwamisha wavuni, akiibua shangwe na nderemo kwa mashabiki wachache waliokuwa kwenye uwanja huo.

Matokeo hayo yanaifanya Stars kukwea juu hadi nafasi ya pili kwenye Kundi F, ikifikisha pointi nne, ikiwa imeshinda mechi moja, sare moja na kufungwa mechi moja.

Kundi hilo linaongozwa na Algeria ambayo juzi ilishinda mechi yake ya tatu mfululizo ikiitwanga Niger mabao 2-1 na kufikisha pointi tisa, Niger ikiwa ya tatu kwa pointi mbili na The Cranes ikiburuza mkia kwa pointi moja.

Dakika 45 za mwanzo, Stars haikufanya mashambulizi yoyote ya hatari zaidi ya faulo mbili zilizopigwa na Novatus Dismas dakika ya 15 mpira ambao ulipaa juu ya lango, na ya 35 ambao ulimpoteza manyoya kipa wa The Cranes, Salim Magoola, lakini haukuingia wavuni.

Mwanzoni dakika ya 12, Stars ilifanya shambulizi jepesi, ambalo Msuva aliambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto na kumimina krosi ambayo ilikatisha katika lango la Waganda hao bila kuwa na muunganishaji.

Kinyume chake, Cranes ilifanikiwa kufanya mashambulizi ya hatari katika lango la Stars kwenye dakika 11, ambapo kona iliyopigwa ilimkuta, Livingston Mulondo aliyeunganisha kwa kichwa, lakini Aishi Manula alikuwa makini, akadaka mpira huo.

Manula tena, dakika ya 24 alilazimika kutoka langoni kwenda mbele kuokoa mpira mrefu uliopigwa na Abdul-Aziz Kayondo, ambao ulikuwa umfikie, Farouk Miya, lakini aliuwahi na kuufagia kabla haujatua mguuni.

Hatari kubwa zaidi ilikuwa dakika ya 29, wakati Joseph Ochoya alipobaki yeye na lango, akipokea krosi kutoka kwa nahodha, Emmanuel Okwi, akapiga shuti ambalo liliwababatiza mabeki wa Stars na kurejea uwanjani, huku kipa Manula

INAENDELEA UK. 23

# Simba SC, Yanga zachanga karata

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuwa tayari kukata tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa, Simba na Yanga zinaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha zinamaliza kwa heshima mechi za makundi za michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Simba inashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika na Machi 31, mwaka huu itakuwa Morocco kuwafuata Raja Casablanca wakati TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) itawaalika Yanga kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema viongozi wa klabu hiyo wamekutana na benchi la ufundi kwa ajili ya kupanga mikakati ya kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na kufanya vyema mchezo wa robo fainali.

Hersi alisema wanataka kuona wanashinda mechi hiyo ya kukamilisha hatua ya makundi kwa sababu itawaongezea nguvu katika hatua inayofuata.

"Tunahitaji kufanya vizuri mechi hiyo na kumaliza kundi tukiendelea kuongoza ili katika hatua inayofuata tupate angalau mpinzani mwenye uwezo wa kawaida. Tayari tumejiandaa kuelekea mchezo huo lakini pia na kuweka mipango yetu ya mechi ijayo ya hatua ya robo fainali, nina imani kuna mambo mazuri na makubwa yanakuja ndani ya klabu yetu," alisema Hersi.

Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, amesema anafurahi kuona amekuwa na msaada mkubwa katika timu yake kuelekea hatua ya robo fainali huku bao lake alilofunga dhidi ya US Monastir ya Tunisia likitangazwa ni goli bora la mzunguko wa tano.

"Kwa sasa niko katika majukumu ya Timu ya Taifa, baada ya michezo hiyo nitaungana na kikosi cha Yanga ambao nitawakuta nyumbani (DRC) kujiandaa na mchezo dhidi ya TP Mazembe, ni muhimu kupata matokeo mbele ya wenyeji wetu," alisema Mayele.

Aliongeza wanafahamu mechi hiyo itakayochezwa Aprili 2, mwaka huu Mjini Lubumbashi itakuwa ngumu kwa sababu wao wataingia na rekodi ya kushinda mechi ya kwanza.

Wakati huo huo, kikosi cha Simba kimeanza mazoezi rasmi kujiwinda kuelekea mchezo wa marudiano dhidi ya Raja Casablanca.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >